Nipashe
Jumatano Agosti 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581033
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US


UCHAGUZI KENYA
Wakenya wamemaliza kazi sasa ni zamu ya shuaa atakayevikwa taji
siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe
MATOKEO UCHAGUZI KENYA
Ni zamu ya kumsubiri anayepindua meza kibabe, kambi ya Ruto, Raila
Kenya wanapomaliza jambo lao kwa amani

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,021,208,577/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO
CHADEMA

**CHADEMA** yatoa mapendekezo ya huduma za NHIF

UKURASA 5

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

UKURASA 11



# Trekta lilivyokata uhai wa watu 20

• **Samia** atuma rambirambi, waliofariki mmoja alikuwa apokee mchezo wa mil. 1.4/-... *Endelea ukurasa 2*







Gari aina ya Toyota Hiace likiwa limegongana uso kwa uso na lori aina ya Scania kwenye eneo hilo na kusababisha vifo vya watu 20 na majeruhi 15. **Picha nyingine;** Gari dogo aina ya Toyota IST, lilipoligonga trekta lililokuwa limeegeshwa kando ya barabara eneo la Mwakata, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga juzi usiku. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Dosari zaripotiwa uchaguzi wa Kenya

UKURASA 2



## Jeneza la Simba laibua maaskofu

UK.3

**MICHEZO** **SIMBA PAGUMU YANGA KWA VIBONDE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mwezeshaji Dastan Kamanzi ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), akitoa mafunzo kuhusu uandishi wa habari wa data kwa waandishi wa IPP Media, yaliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, katika ofisi za TGL Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Ajali yakatisha uhai watu 20

**Na Waandishi Wetu,** KAHAMA

WATU 20 wamefariki dunia na wengine 15 kujeruhiwa kwenye ajali iliyohusisha magari mawili na trekta katika eneo la Mwakata Halmashauri ya Msalala barabara itokayo mji mdogo wa Isaka kwenda wilayani Kahama, usiku wa kuamkia jana.

Ajali hiyo imehusisha Toyota IST yenye namba za usajili T 880 DUE, Hiace, T 350 BDX na lori aina ya Scania, T 658 DUW, baada ya kugongana uso kwa uso.

**RAIS ATUMA RAMBIRAMBI**

Kutokana na ajali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, ilisema Rais Samia ametoa pole kwa wafiwa na kuungana na familia hizo katika kipindi hiki kigumu, huku akiagiza vyombo vinavyosimamia usalama barabarani kuongeza juhudi kudhibiti ajali.

**DAKTARI ATHIBITISHA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Deogratius Nyaga, alithibitisha kupokea miili ya watu 20 na majeruhi 15 ambao wanaendelea na matibabu huku miili ikihifadhiwa chumba cha maiti.

Nyaga alisema kati ya majeruhi 15, watatu watapewa rufani ya kwenda kupata matibabu zaidi katika Hospitali ya Shinyanga au Bugando, mkoani Mwanza, kwa sasa wamepelekwa kwenye vipimo vya X-Ray kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kabla ya kuhamishwa.

"Tumepokea jumla ya miili 20 ya marehemu wa ajali hii na majeruhi 15 na kati ya hao watatu hali zao ni mbaya, tunatarajia kuwapatia rufani kwa ajili ya matibabu zaidi katika hospitali za rufani za Shinyanga au Bugando mkoani Mwanza," alisema Nyaga.

Dk. Nyaga alisema kati ya waliofariki wanawake ni watatu na wanaume 17. Alisema majeruhi Daines Haule, amevunjika mkono wa kulia na mapaja yote mawili anatarajiwa kupewa rufani kwenda Shinyanga au Bugando na mume wake amepata majeraha kichwani anafanyiwa uchunguzi.

Akitaja baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo, Dk. Nyaga alisema ni Paul Sebstania (44), Omary Shabani (26), Kulwa Omary (17), Mahubi Tembo (29), Joseph Tumaini (37), Ally Emmanuel (18), Paschal Joseph (32), Simon John (40), Hamisi George (29), Daines Haule (43), Mwasiti Samweli (23) na Salome Silime (37).

Alisema, kati ya waliofariki 17 walikuwa wanaume na watatu wanawake na wanaendelea kutambuliwa kwa majina yao baada ya ndugu jamaa na marafiki kujitokeza na kutambua miili ya wapendwa wao waliopata ajali hiyo.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, ACP Leonard Nyandahu, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo saa 4.35 usiku wa kuamkia jana katika eneo la Kata ya Mwakata-Msalala na kusema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa madereva wote ambao hawakuchukua tahadhari wawapo katika vyombo hivyo.

Alisema, kulitokea ajali mbili tofauti, ya kwanza ilihusisha trekta iliyokuwa imesimama pembezoni mwa barabara bila kuwapo kwa viashiria kuonyesha kusimama hali iliyosababisha gari dogo aina ya Toyota IST kugonga nyuma na kusababisha vifo.

Aidha, ACP Nyandahu alisema, ajali ya pili ilihusisha Toyota Hiace iliyokuwa ikitokea wilayani Kahama kuelekea Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, baada ya kugongana uso kwa uso na lori wakati likijaribu kukwepa ajali ya IST na trekta.

Aliwataka madereva kuchukua tahadhari kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa kuangalia alama ili kuepusha ajali zinazopoteza maisha ya Watanzania kwa uzembe wao.

Alisema katika gari ya IST walikuta chupa ya pombe.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Mabula Chande alisema, ajali hiyo ni mbaya ambayo haijawahi kutokea katika eneo hilo huku akiwataka madereva kuwa makini wawapo barabarani, kwa kuwa eneo hilo limekuwa na mikokoteni mingi inayovutwa na punda nyakati za usiku.

Majeruhi Salome Silime alisema, alikuwa akitoka Wilaya ya Masumbwe mkoani Geita akielekea mkoani Shinyanga na walipofika kwenye Kata ya Mwakata waligongana uso kwa uso na lori na kumsababishia kuvunjika miguu yote miwili.

Majeruhi Simon John, alisema mwendo wa gari aina ya Haice aliyokuwa amepanda akitoka kwenye kikao Kahama akielekea Tinde, ulikuwa wa kawaida isipokuwa wakati wanakwepa ajali iliyokuwa imetokea awali eneo hilo la Mwakata, waligongana na lori hali iliyosababisha apoteze fahamu na kujikuta hospitalini.

**MKE ASIMULIA MUME ALIVYOMUAGA**

Mariamu Musa, mke wa mmoja wa marehemu aliyetambuliwa kwenye ajali hiyo, Musa Ally, maarufu (weusi) aliyekuwa akifanya kazi ya ufundi wa magari katika gereji ya Nyihogo, wilayani Kahama, alisema mume wake alimuaga asubuhi kuwa anaenda kazini, lakini alikuwa anajisikia vibaya.

Mariamu alimwambia mwandishi wa habari hizi jana kuwa alimtambua mume wake kwa nguo alizokuwa amevaa na rangi yake baada ya kupigiwa simu na bibi wa marehemu mume wake kwenda chumba cha kuhifadhia maiti kutambua maiti.

Alisema alikwenda kuutambua mwili akiwa na wafanyakazi wenzake marehemu na kuthibitisha kuwa ni yeye na kwamba walifunga ndoa mwaka jana na kubahatika kupata mtoto mmoja.

Mama mdogo wa marehemu, Kaisiki Majid, mfanyakazi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wilayani Kahama, alisema alimlea Ally tangu akiwa mtoto baada ya mama yake mzazi kufariki na kumuacha akiwa mdogo.

Alisema, amemlea na kumsomesha mpaka alipofunga ndoa mwaka jana na kuondoka mikononi mwake.

Vicent Jackson, mfanyakazi mwenzie katika gereji hiyo alisema kuwa Ally aliondoka gereji majira ya saa moja jioni baada ya kuchukuliwa na tajiri wa gari ndogo aina IST kwa ajili ya kwenda kutengeneza Scania eneo la Isaka.

**ILIKUWA APOKEE MCHEZO WA MIL. 1.4**

"Leo hii marehemu ilikuwa zamu yake ya kupokea mchezo kiasi cha Sh. milioni 1.4, lakini hajarudi kuja kuzipokea, niliposikia kuwa kuna ajali sikujua kama angekuwamo na yeye tulipata taarifa kuwa alikuwa anarudi Kahama majira saa nne baada ya kumaliza kazi Isaka," alisema Jackson.

Mmoja wa majeruhi aliyelazwa hospitali ya wilaya, Paul Sebastian (35), aliyekuwa kwenye gari aina ya Hiace alisema kuwa gari ndogo aina ya IST aliiona ikigonga semitrailer baada ya kuipita Hiace ikiwa mwendo kasi.

***Imeandikwa na Shaaban Njia na Neema Sakawa (KAHAMA)**

## Dosari zaripotiwa Uchaguzi Kenya

**Na Maulid Mmbaga**

DOSARI mbalimbali zimeripotiwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika jana, baadhi ya wananchi wakidaiwa kushindwa kupiga kura, karatasi kukosekana huku idadi ya wapigakura ikipungua.

Vilevile, imeripotiwa na vyombo vya habari kwamba katika baadhi ya maeneo, wapigakura walilala kwenye vituo ili kuwahi nafasi ya kutimiza wajibu wao wa kikatiba jana.

Katika uchaguzi huo takribani watu milioni 20 walijiandikisha kwenye zaidi ya vituo 46,232 walikuwa wanachagua Rais, magavana, maseneta wabunge, wawakilishi wa wanawake na wawakilishi wa mabunge ya kaunti.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na DW, idadi ya wapigakura inaripotiwa kuwa chini kulinganishwa na uchaguzi uliopita.

Ilibainishwa kuwa baadhi ya wananchi wanadaiwa kulała vituoni ili kuwahi kupiga kura huku wanawake wakiwa wamebeba watoto wakiwa kwenye mistari ya kusubiri kutimiza wajibu wa kikatiba.

Taarifa hiyo ilibainisha kwamba baadhi ya wananchi waliojitokeza kupiga kura katika vituo vya eneo la Rongai huko Nakuru, waligundua kuwa majina ya wagombea wa viti vya bunge la kitaifa kwenye eneo hilo hayakuwapo.

Mmoja wa wagombea katika eneo hilo ni Mbunge Raymond Moi, mtoto wa Rais wa Pili wa Kenya, Hayati Daniel Moi, alionyesha kutoridhishwa na dosari zilizojitokeza kinyume cha taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati, kwamba maandalizi yalikuwa tayari na uchaguzi utakuwa huru.

"Nimeshangaa sana nilipojaribu kupiga kura na nikajikuta siko kwenye karatasi ya kupigia kura, huu ni uzembe wa aina gani? Mwenyekiti alituhakikishia wako tayari, lakini hawako tayari, jambo kama hilo limefanyika kule Kacheliba, limefanyika Pokot Magharibi," alilalamika Raymond.

Pia, wananchi kwenye kituo cha kupigia kura mjini Nairobi, walionyesha kukasirishwa baada ya shughuli ya kupiga kura kutokuanza kwa wakati.

Ofisa Mkuu wa IEBC eneo la Nakuru, Joseph Mele, alisema hilo ni jambo linaloshughulikiwa na usimamizi wa tume hiyo ya IEBC.

Pia, inaripotiwa kuwa kumekuwapo na malalamiko ya kukosekana kwa taarifa za baadhi ya wapigakura kwenye vifaa vya kupiga kura.

Gavana wa Nakuru Lee Kinyanjui, alibainisha kuwa vituo vya kupigia kura eneo hilo vilionekana kuwa na idadi ndogo ya wapigakura, hasa kundi la vijana ambao walionekana kushabikia mikutano ya kampeni za siasa.

"Kuna muda bado, tungependa watu wajitokeze, kama taifa tumetumia mabilioni ya shilingi kuandaa suala hili, kwa hiyo idadi ikiwa chache ni uharibifu mkubwa wa fedha za umma," alisema Kinyanjui.

Gavana Kinyanjui anakitetea kiti chake dhidi ya mpinzani wake Susana Kihika wa chama cha UDA.

Kwa mujibu wa BBC, ulinzi umeimarishwa kote Kenya huku maofisa 150,000 wakipiga doria kuzuia uwezekano wowote wa machafuko.

Mwenyekiti wa IEBC Chebukati, alisema jumla ya vituo 46,232 vimesajiliwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.08 kutoka vituo 40,883 vya miaka mitano iliyopita.

Alisema waliojiandikisha wameongezeka kutoka 19,611,423 hadi 22,120,458, sawa na asilimia 12.79, huku baadhi ya maeneo yakionekana kuwa na wapigakura wachache.

Tume hiyo imeahidi kumtangaza mshindi wa urais ndani ya siku saba na kwamba itakuwa ni mchana tofauti na miaka mingine alitangazwa usiku.

Wagombea wa urais katika uchaguzi huo na vyama vyao kwenye mabano ni Raila Odinga (Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya maarufu kama Azimio Coalition) aliyepigia kura kituo cha Gichungu kilichopo Kirinyaga, William Ruto (Chama cha United Democratic Alliance (UDA) maarufu kama Kenya Kwanza Coalition), aliyepiga kura eneo la Sugoi Jimbo la Bonde la Ufa.

Wagombe wengine ni wa Chama cha Roots, Prof. George Wajackoya, na Waure Waohiga wa Chama cha Agano.

HABARI KITAIFA

# Jeneza la Simba laibua maaskofu

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa dini wakiwamo maaskofu, wameibuka na kutoa kauli kuhusu kitendo cha klabu ya Simba kuingiza jeneza lililokuwa limembeba msanii Tunda Man.

Tukio hilo lilitokea juzi katika Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam, wakati wa tamasha la Siku ya Simba. Watu waliokuwa wamevalia nguo nyeusi walibeba jeneza na kuingia nalo mlangoni pamoja na msalaba na shabiki mmoja akiwa amevalia joho jeusi na stola nyekundu akiwa na Biblia mkononi.

Baada ya kufika katikati ya uwanja, alitoa maelezo kwamba ndani ya jeneza hilo kuna mtu aliyefariki dunia Agosti 6, mwaka huu katika uwanja huo na chanzo cha kifo chake ni kuponzwa na mdomo. Jumamosi, Yanga ilihitimisha Wiki ya Wananchi kwa kucheza na Vipers ya Uganda na kufungwa mabao 2-0.

Kutokana na kitendo hicho, viongozi wa dini na wadau mbalimbali wameibuka na kushutumu kitendo hicho huku baadhi yao wakisema ni dhihaka dhidi ya dini ya Kikristo na kinapaswa kulaaniwa.

Askofu Msaidizi wa Kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba, Dk. Methodius Kilaini, alisema kitendo hicho ni kibaya na kinapaswa kukemewa.

Kwa mujibu wa Askofu Kilaini, kitendo hicho ni cha kudhalilisha dini pamoja na imani za watu wengine na kwamba atawasiliana na viongozi wenzake ili kuona namna gani watalikemea ili lisitokee tena.

"Hiki ni kitendo kibaya ambacho kinadhalilisha dini na imani za watu. Hakipaswi kuendelea kuwapo kwa mara nyingine hata kama ni masuala ya michezo," alisema Askofu Kilaini,



Naye Askofu wa Tanzania Assemblies of God (TAG), Jimbo la Kigoma, Mulenda Kalama, alisema kitendo hicho ni kibaya na kwamba kinaashiria jambo baya kutokea.

Alisema kitendo hicho kinaashiria kuwapo pia maafa katika siku zijazo katika maeneo hayo ya mpira.

Hiki ni kitendo kibaya ambacho kinapaswa kukemewa na kila mtu. Hata kama ni masuala ya mpira, huwezi kubeba jeneza na ukaweka msalaba juu," alisema.

Naye mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema kitendo hicho hakikubaliki na kusisitiza kuwa: "Huyu dogo (Tunda Man) kajitabiria mwisho wake, ni suala la muda tu."

**WADAU WAFUNGUKA**

Baadhi ya mashabiki na wadau walitoa maoni yao huku wengi wakionyesha kutokuafiki kitendo hicho huku wakisema kitendo hicho ni kumdhihaki Mungu na kwamba badala ya kuweka mikakati ya kuchukua makombe, wao wanadhihaki dini za watu wengine.

Katika ukurasa wa Facebook, mdau mmoja aliyejitambulisha kwa jina la MC Mwangata aliandika: "Ninauheshimu sana msalaba. Kwa hili sijapenda aisee, huu ubunifu sijaupenda na umekwaza wengi."

Mary Lyimo katika ujumbe wake aliouandika kwenye mtandao huo, alionyesha kusikitishwa na kitendo hicho huku akisema msalaba una thamani kubwa kwa Wakristo.

Naye Abdallah Bawazir aliandika: "Imani ya dini inapotumika katika sanaa kueneza neno la Mungu, kufundisha, kuonya au kuongoa watu ni sawa na haina tatizo kabisa. Lakini inapotumika katika sanaa kudhihaki, kukera wengine, kukejeli au kinyume cha lengo lake si sawa na inapaswa kukemewa na kila anayejitambua."

Mkuu wa Wilaya Mstaafu, Betty Mkwasa, aliandika kuwa: "Kwenye hili hatunyamazi asilani! This is too much'. Alama ya msalaba ina maana kubwa sana kwetu (Wakristo). Mnawafundisha nini vizazi vijavyo? Upuuzi huu na ukome."

Mdau mwingine, Edmund Mihale, katika ukurasa wake wa Facebook aliandika: Mie ni Simba damu lakini linapokuja suala la imani yangu ya Ukristo, Simba ni takataka. Kitendo kilichofanywa jana (juzi) na Simba kimedhalilisha na kupuuza msalaba ambao kwetu sisi Wakristo ni ishara ya ukombozi wetu."

## Makada 155 CCM wachuana ubunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

PAZIA la uchukuaji fomu za kuomba kuwania ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) linafungwa leo ili kuruhusu michakato mingine ndani ya chama kuendelea.

Hadi jana, makada 155 wa chama hicho walikuwa wamechukua fomu, ikiwa ni ishara ya kuwapo mchuano mkali kutokana na nafasi hiyo kuhitaji watu tisa wakiwamo wawakilishi kutoka vyama vya upinzani.

Akitoa taarifa ya uchukuaji fomu, Katibu wa NEC, Organaizesheni wa CCM, Dk. Maudline Castico, alisema jana kuwa uchukuaji fomu ulianza Agosti Mosi na mwisho ni Agosti 10 mwaka huu, yaani leo.

Aliwataja wanachama hao ni Doto Nanauka, Sahila Wilfref, Evangel Otieno, Malema Eli, Loman Mollel, Joel Nanauka, John Haule, Lameck Jaston, Mwamvua Sykes, Bashira Nabhaniy, Diana Obare, Arafa Mashi, Baltazar Awe, Frank Mbele, Fredy Katembo na Yussuf Suleiman Khalfan.

Vilevile, Suzana Kabula, Itikija Mwanga, Neema Mwinge, Getrude Haule, Lwitiko Anyingyisye, Salum Kanyungu, Edna Mafuwe, Dk Salvatory Mhando, Godfrey Simbeye, Elias Komba, Consolata Mulalo, Lunus Linda, Lathifa Skyes, Dk Hamad Juma, Fatma Omar.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

BEI YA MBOLEA YA RUZUKU KWA WAKULIMA

**10 AGOSTI, 2022 – DAR ES SALAAM**

Kutokana na kupanda kwa bei za mbolea katika soko la dunia na hapa nchini, Serikali imepanga na imetenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea itakayotolewa kwa wakulima wote nchini kwa lengo la kuwapunguzia makali ya bei. Mbolea zitakazohusika kwenye mpango wa ruzuku ni mbolea za kupandia na kukuzia kulingana na mahitaji ya soko.

Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea umezinduliwa rasmi na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 08/08/2022 jijini Mbeya katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima maarufu kama Nanenane. Katika uzinduzi wa mpago huo, Mhe. Rais alielekeza wakulima kuanza kununua mbolea kwa bei ya ruzuku ifikapo tarehe 15/08/2022.

Wastani wa bei za mbolea katika mpango wa ruzuku utakuwa ni kama ifuatavyo:-

| AINA YA MBOLEA | WASTANI WA BEI YA MBOLEA BILA RUZUKU | BEI YA MBOLEA YA RUZUKU | RUZUKU YA SERIKALI |
|---|---|---|---|
| DAP | 131,676 | 70,000 | 61,676 |
| UREA | 124,734 | 70,000 | 54,734 |
| CAN | 108,156 | 60,000 | 48,156 |
| SA | 82,852 | 50,000 | 32,852 |
| NPKs | 122,695 | 70,000 | 52,695 |

Aidha zoezi la usajili wa wakulima kwa ajili ya kunufaika na ruzuku iliyotolewa na Serikali unaendelea katika nchini kote.

**Kwa mawasiliano tafadhali piga namba hii BURE 0733 800200.**

Dkt. Stephan E. Ngailo
**MKURUGENZI MTENDAJI**

*Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*

Kilimo Street, Kilimo I Complex Building, P.O. Box 46238, 15471 Dar es salaam.
Tel: +255 22 2861939, E-mail: info@tfra.go.tz, Website: www.tfra.go.tz
All correspondence should be addressed to The Executive Director.

216982902



TOL Gases Limited
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

NOTICE

2021 ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited for the year ended December, 31, 2021 will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 19th August, 2022 at 9.00 am to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2020 Annual General Meeting held on 27th August, 2021.
3. Matters arising from minutes of the year 2020 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive the Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December 31, 2021.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2022.
9. Amendment of MEMARTS
10. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

A member entitled to attend and vote at the Meeting is entitled to appoint any person (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz /nlulu@tol.gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIOUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.Kitoka – (Tanzanian)

216982401

RIPOTI MAALUM -4

## KIBORIANI

# Shule yenye mazingira hatarishi kwa wanafunzi, walimu na elimu

Na Sanula Athanas

**KATIKA sehemu ya tatu ya ripoti hii jana, kulikuwa na ushuhuda wa ugumu wa ufundishaji na ujifunzaji katika Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma. Endelea na sehemu ya mwisho kupata undani wa mustakabali wake.**

---

Baada ya kupatikana ufafanuzi wa kina kijijini Kiboriani kuhusu madhila ya elimu shuleni hapo, safari ya Nipashe inashuka Km 21 na kurejea bondeni mjini kwenye ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kupata ufafanuzi wa wasimamizi wakuu wa kituo hicho cha elimu kinachochechemea.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Mpwapwa, Egidio Fungafunga, naye anaingia katika mnyororo wa kukiri kujua matatizo hayo, akitanguliza utetezi katika mwaka wa fedha uliopo, madarasa mawili mapya yako mbioni kujengwa shuleni Kiboriani.

Hata hivyo, kuhusu matatizo mengine ya uhaba wa walimu, hali mbaya ya vyoo, madawati na nyumba za walimu, Fungafunga anasema liko nje ya uwezo wao na hatua waliyochukua ni kuwasilisha kilio hicho wizarani (TAMISEMI) kupata usaidizi.

Ofisa Elimu huyo pia anaeleza kuhusu uhaba wa walimu kwamba wanavyopangwa ni nje ya uwezo wao, wanaletewa wakiwa wamepangiwa vituo vya kazi. Ndivyo ilivyo hata kwenye mpangilio wa uwiano kijinsia kazini.

Kuhusu usalama wa mitihani kwa shule hiyo iliyoko mlimani, Fungafunga anasema kuna hatua za ziada zinazojumuisha kuwa na maofisa maalum wa kiserikali, wakiipeleka huko mapema na kusimamia usalama wake.

Nipashe pia inatua mezani kwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Dismas Pesambili, anayebainisha hatua walizochukua kunusuru vyoo shuleni Kiboriani.

Anasema katika kipindi kilichoko ambacho wana hali mbaya kibajeti, wamepanga kuchukua Sh. milioni 2.5 kwenye Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kunusuru vyoo vya shule hiyo huku wakisubiri msaada zaidi wa mamlaka za juu serikalini kuisaidia Shule ya Msingi Kiboriani na baadhi ya shule zingine ambazo zinaunda jumla ya shule za msingi 122 wilayani Mpwapwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ambaye ni Diwani wa Kata ya Mpwapwa Mjini inakopatikana Shule ya Msingi Kiboriani, George Fuime, anasema mkakati wa kijiji kupata kibali cha TFS kukata miti ya kutengeneza madawati, umeshapata ufumbuzi kwa kukubaliwa.

Anasema hatua iliyobaki ni uwezo wa kifedha wa kugharamia matengenezo ya madawati kwa ajili ya shule hiyo.

Kutokana na funzo la Kiboriani na shule zinginezo zenye shida, Fuime anasema Baraza la Madiwani limebaini bajeti kutoka Serikali Kuu kukidhi mahitaji kama hayo ni ndogo, hivyo wako mbioni kutunga sheria ndogo itakayowaruhusu kuwa na bajeti zaidi ya kushughulikia shida za namna hiyo.

**MWITIKIO TAMISEMI**

Baada ya Nipashe kujitosheleza na ufafanuzi kutoka ngazi ya wilaya, ikagonga hodi kwa msimamizi mkuu ambaye ni Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ikizingatiwa baadhi ya hoja zimesogezwa mezani kwake na anapaswa kuwajibika nazo.



Nyumba pekee iliyojengwa na serikali kwa ajili ya makazi ya walimu katika Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa. **PICHA: SANULA ATHANAS**

Nteghenjwa Hosseah, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwanza anakiri fika kufahamu madhila yaliyomo ndani ya Shule ya Msingi Kiboriani.

Kipi kinachofanyika? Hapo ofisa huyo anaendelea kutoa ufafanuzi kwamba hatua za haraka kukabili shida zilizopo sasa zinachukuliwa zikiwa katika sura kuu tatu.

Ya kwanza ofisa huyo anasema katika kilio kikuu cha vyoo kwa mwaka uliopo wa fedha wanatarajia kujenga matundu sita ya vyoo sambamba na vyumba viwili vya madarasa kukabili hali mbaya ya miundombinu shuleni.

Ofisa huyo alitaja hatua ya pili kwamba kutafanyika uhamisho wa haraka wa mwalimu wa kike kwenda shuleni Kiboriani.

Kwa mujibu wa msemaji huyo, hatua hizo zinafanyika kulingana na uwezo wa bajeti uliopo sasa kupitia mradi anaoutambulisha kwa jina la BOOST unaotumika kukabili kasoro zinazojitokeza kama hizo.

Msemaji huyo anaitaja hatua ya tatu ni pale TAMISEMI imeshirikisha wadau wake wa elimu, ikiwamo HakiElimu, kujumuika katika mkakati wa kuinusuru Kiboriani, akiithibitishia Nipashe kwamba taasisi hiyo isiyo ya kiserikali tayari imeshaweka kwenye orodha ya mikakati yake ya haraka kutafuta uwezekano wa kuisaidia shule hiyo, nayo ikitumia mtandao wake mpana katika uwekezaji na maboresho ya elimu wilayani Mpwapwa.

"Serikali inatoa fedha kupitia mradi wa BOOST. Maelekezo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni ufanyike msawazo wa walimu. Kuna shule jirani na Kiboriani zina walimu wengi, tumeagiza kusiwe na mrundikano mkubwa wa walimu kwenye shule moja ilhali shule zingine zina uhaba," Nteghenjwa anahitimisha.

**JICHO LA CAG**

Kimsingi, Shule ya Msingi Kiboriani kuwa katika hali mbaya kimiundombinu na rasilimali watu ni ishara ya kutotekelezwa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Aprili 2017.

**"Ni wazi kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu hawakutekeleza mapendekezo yangu ya mwaka 2017..."**

Kwenye ripoti yake kuhusu Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani katika Shule za Msingi nchini, CAG (wakati huo Prof. Mussa Assad) alibaini hali mbaya ya miundombinu na uhaba wa samani na walimu shuleni, Shule ya Msingi Kiboriani ikiwa sehemu ya zilizofikiwa na ukaguzi huo.

**RIPOTI MPYA**

Aprili 12, mwaka huu, CAG mpya, Charles Kichere (pichani), alitoa taarifa mpya kuhusu suala hilo aliyoipa jina la Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji Mapendekezo ya Ukaguzi Maalum wa Mwaka 2017, akibainisha kuwa katika halmashauri 48 alizozifikia, ikiwamo Mpwapwa, amebaini kati ya walimu 40,458 wanaohitajika kwenye shule za msingi, walipo ni 23,881, ikiwa na tafsiri ya kuwapo uhaba wa walimu 16,571, sawa na asilimia 41 huku uboreshaji wa miundombinu nao ukisuasua.



CAG pia anabainisha dosari mpya aliyoibaini ya kuwapo shule za msingi ambazo zimesajiliwa licha ya kutokidhi vigezo vinavyojumuisha ubora na usalama wa miundombinu inayotakiwa kisera.

Anasema takriban wanafunzi milioni nne (asilimia 48), hawana vyumba vya madarasa huku milioni 5.4 (asilimia 65) hawana huduma ya choo shuleni, kwa kuzingatia uwiano uliowekwa kisera; yaani wanafunzi 45 kwa kila chumba cha darasa na wavulana 25 kwa kila tundu la choo na wasichana 20 kwa kila tundu la choo.

Vilevile, katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12 mwaka huu, CAG Kichere anabainisha kuwa halmashauri 77 zina uhaba wa vyumba vya madarasa 74,735, nyumba za walimu 73,135, ofisi za walimu 5,112, viti 65,889, meza 185,840 na matundu ya vyoo 111,931, akipendekeza serikali ichukue hatua za haraka kuboresha miundombinu iliyopo na kujenga mipya sambamba na kuajiri walimu wapya.

| Vifaa | Mahitaji | Vilivyopo | Uhaba |
|---|---|---|---|
| Madarasa | 124,268 | 49,533 | 74,735 |
| Nyumba | 90,742 | 17,607 | 73,135 |
| Ofisi | 9,730 | 4,618 | 5,112 |
| Viti | 150,833 | 84,944 | 65,889 |
| Meza | 632,062 | 446,222 | 185,840 |
| Vyoo | 178,54 | 66,616 | 111,931 |

**Hali ya uhaba wa miundombinu na samani katika halmashauri 77 nchini. CHANZO: RIPOTI YA CAG 2020/21**

Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 pia inaelekeza kila mwalimu apate nyumba yake inayojitegemea, jambo ambalo hali iliyopo Kiboriani bado ni mbali kufikiwa katika mtazamo wa sera, shule hiyo ikiwa na nyumba moja tu iliyojengwa na serikali kwa ajili ya makazi ya walimu.

"Kwa kuzingatia uchambuzi huu, ni wazi kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hawakutekeleza kikamilifu mapendekezo yangu ya mwaka 2017.

"Hii inaweza kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia ufaulu duni wa wanafunzi wa shule za msingi nchini. Hali hii inadidimiza juhudi za serikali katika kuboresha elimu ya msingi na sekondari," CAG Kichere anabainisha.

**NINI KIFANYIKE?**

CAG Kichere anapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wafanye tathmini kuhusu dosari alizozibaini ili kuboresha elimu ya msingi.

Kwa mujibu wa CAG, hilo litawezekana ikiwa Hazina itatoa fedha za kutosha na kuweka mikakati inayotekelezeka ili kukabiliana na upungufu uliobainika.

"Ofisi ya Rais - TAMISEMI pia itafute kibali cha ajira za walimu kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuziba pengo lililoko," CAG Kichere anashauri.

Katika uchunguzi wake, Nipashe imebaini uhaba na uchakavu wa miundombinu kwenye Shule ya Msingi Kiboriani, pia unazikabili shule zingine za msingi wilayani Mpwapwa, zikiwamo Kikombo, Nana na Mang'aliza.

## HABARI KITAIFA

# DPP atoa ushahidi kesi waliodai usalama wa taifa

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, amepanda kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam katika kesi ya watu wawili waliojitambulisha kuwa maofisa wa Usalama wa Taifa.

Katika ushahidi wake alioutoa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate, Mwakitalu alidai kuwa watu hao, Joshua Kamalamo na Yahya Kapalatu, walimtaka asitishe majadiliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Herbender Seth na wenzake.

Akiongonzwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hilla, Mwakitalu alidai kwamba Juni 11, mwaka jana, akiwa kwenye ofisi ndogo ya Dar es Salaam, alipigiwa simu na msaidizi wake, Joseph Pande, saa 2:00 usiku kuwa kuna watu wanataka kuonana naye wametoka ofisi ya Rais ni Idara ya Usalama wa Taifa (TISS).

Alidai kwamba muda huo alikuwa bado yuko ofisini, kutokana na kazi nyingi alizokuwa nazo, aliwaeleza kwamba waende wakaonane naye kesho ambayo ilikuwa Jumamosi saa 2:00 asubuhi ili awasikilize.

Pia alidai kuwa alitoa maelekezo kwa Pande kwamba awapatie watu hao namba zake za simu ili wakipotea wampigie na kwamba siku hiyo ya miadi alifika ofisini saa 1:00 asubuhi ofisini kwake.

"Muda ambao tulikubaliana saa 2:00 asubuhi walifika wanaume wawili nikawapokea, tukasalimiana tukaingia ofisini kwangu nikawaambia niko tayari kuwasikiliza, wakajitambulisha majina yao kwamba wanatoka ofisi ya Rais. "Joshua alijitambulisha kuwa kazi yake iko Makumbusho na anatoka Ofisi ya Rais na mwingine Yahya alisema anatoka Kampuni ya Pan African Power Solutions Ltd (PAP) iliyoko Tegeta, Dar es Salaam ambapo yeye amependikizwa kwenye kampuni hii, " alidai DPP Mwakitalu.

Alidai kuwa hawakutaja kazi zao bali walidai wao ni Usalama wa Taifa wameelekezwa wasitishe majadiliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi yanayoendelea baina ya Seth na wenzake hadi watakapopewa maelekezo kwa sababu wana mambo mengi kutoka Ikulu.

# CHADEMA yatoa mapendekezo NHIF

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa mapendekezo nane kwa serikali kuhusu utendaji kazi, usimamizi na uendeshwaji wa mifuko ya bima ya afya nchini ikiwamo kupitia upya na kufanya mabadiliko ya Sera ya Afya ya Taifa ili iendane na wakati ulioko.

Mapendekezo hayo yamekuja baada ya chama hicho kubaini upungufu katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kikidai kuwapo ubaguzi wa kimatibabu kwa wananchi na uhaba wa wataalamu na migogoro kati ya mfuko na watoa huduma za afya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Huduma za Jamii wa CHADEMA, Ashura Masoud, pendekezo la pili ni kuanzishwa mjadala wa kitaifa wa wadau wa afya na watumiaji wa bima ya NHIF kuhusu kufanya maboresho endelevu ya mfuko huo.

"La tatu, kuzuia mabadiliko au matamko yanayolenga kubadili upatikanaji wa huduma za afya kupitia NHIF mpaka ushirikishwaji wa wanachama wa mfuko utakapofanyika," alisema.

Kadhalika, alisema pendekezo la nne ni kubadili haraka mfumo wa usimamizi wa NHIF, kuwapo usimamizi wa kutosha katika kupanga na kutekeleza mabadiliko yoyote yanayoathiri wanachama au watumiaji wa mfuko na sio kusubiri mpaka mabadiliko yafanyike ndiyo mamlaka za juu ziingilie na kuepusha athari zinazoweza kuepukika.

Pendekezo la tano ni Wizara ya Afya kuweka mdhibiti wa huduma za Bima ya Afya na kwamba wanamuunga mkono Waziri wa Afya Ummy Mwalimu kwa kutoa maelekezo ya kuwapo mdhibiti huyo ambaye kazi yake itakuwa ni kuhakiki huduma zinazotolewa. Pia, alishauri kuundwe tume ya usuluhishi itakayoshughulikia migogoro kati ya mtoa huduma na wanachama.

Pendekezo la saba ni wizara isiishie kuweka tume ya usuluhishi migogoro baina ya watoa huduma na watumiaji wa bima, badala yake msuluhishi asuluhishe migogoro iliyoko kati ya mfuko wa NHIF na watoa huduma ya afya.

"Takwimu inaonesha kutokana na maoni ya wadau, mgogoro mkubwa upo kati ya NHIF na watoa huduma hasa unaotokana na kucheleweshewa malipo na kukatiwa kiasi cha fedha kwenye madai yao.

Pendekezo la nane, aliishauri wizara iweke juhudi za kuajiri wafanyakazi wa kutosha kulingana utaratibu husika kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya hadi hospitali za rufani ili kuondoa uhaba wa wafanyakazi.

Alisema hiyo itarahisisha katika utoaji wa huduma za kimatibabu kwa wagonjwa wote wenye bima na wasiokuwa nayo.

"Zahanati za huko vijijini mfano kutoka Wilaya ya Kakonko kuna mkunga mmoja na mganga mmoja hao wanalazimika kupokea wagonjwa, kuwasikiliza, kuwaandikia, kupima, kuandika dawa, kupokea watu wa Bima na kutoa dawa," alibainisha Masoud.

Aidha, alisema taarifa inaonyesha NHIF uwezo wake unapungua kwa asilimia tano kila mwaka, akidai kwamba mwelekeo wa mfuko huo ni mbaya kwa kuwa utashindwa kujiendesha na kufilisika siku za usoni.

Alidai mpaka sasa ni asilimia saba ya wananchi ndiyo watumiaji wa bima ya NHIF nchini na kwamba umepoteza uimara wa ndani kutokana na kuelekea kushindwa kujisimamia na kujiendesha.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MASS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | LILIAN FRANCIS MBETWA | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 100986,KIWANJA NAMBA 70 KITALU '18' | LEILA FRANCIS KAMA MLEZI WA AMIRI HAMISI IDD | MAGOMENI | 24/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | OSCAR EMMANUEL MHEMBANO | NYUMBA | OSCAR EMMANUEL MHEMBANO | NTYUKA-DODOMA | 26/08/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | IBRAHIM WILIAM MKWAWA | NYUMBA | IBRAHIM WILIAM MKWAWA | CHALINZE NYAMA-DODOMA | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NUNDU ILEMELA -MWANZA | 29/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | RESA ROOFERS | NYUMBA | SAMUEL CHRISTOPHER RICHARD | NYAKATO-MWANZA | 30/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | NYUMBA | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | GOBA MATOSA | 28/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MARIAM JUMANNE ULEDI | NYUMBA | MARIAM JUMANNE ULEDI | KINYEREZI KANGA-TABATA | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | THOBIAS ERNES ASSENGA | NYUMBA | THOBIAS ERNES ASSENGA | MBEZI MSUMI | 30/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MARIAM PATRICK SHAYO | NYUMBA | DORICE YOHANA MWAKAPESA | MBEZI MSAKUZI | 30/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ABIUDI ADRIAN KIMARIO | KIWANJA | ABIUDI ADRIAN KIMARIO | KIBAHA | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SUBILAGA SELEMANI LUGANGA | NYUMBA | SUBILAGA SELEMANI LUGANGA | MBEZI MTONI | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | FELIX BIRCKMAS ALOYS | MBEZI KWA YUSUFU | 28/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | RASCAR AUTO WORKS | NYUMBA | OSCAR BENALD NG'ITTU | MBEZI MTONI | 24/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SELEMANI HEMEDI RAMADHANI | NYUMBA | SELEMANI HEMEDI RAMADHANI | GOBA KINZUDI | 25/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BOSCO BONIFACE KABAKAMA | NYUMBA | BOSCO BONIFACE KABAKAMA | BOKO BASIHAYA | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | IPYANA GIDEON TUNTUFYE | NYUMBA | IPYANA GIDEON TUNTUFYE | KIMARA' B' SARANGA | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | KELVINI RABSON SWAI | NYUMBA | CALVIN RABSON SWAI | BUNJU 'B' | 25/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ABDUL SALEHE ABDALLAH | NYUMBA | ABDUL SALEHE ABDALLAH | MBWENI | 25/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JASTINI LEONARD VYALELO | NYUMBA | JASTINI LEONARD VYALELO | GOBA KINZUDI | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | IBRAHIM BYSON MWANSULE | NYUMBA | IBRAHIM BYSON MWANSULE | BUNJU 'B' | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | EWALD EDWARD TEMBA | NYUMBA | TATU MOHAMED NGARONGA | JONGO-MAKURUMLA | 27/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | FATUMA ATHUMAN MBARUKU | NYUMBA | EMELDA E MPAGAMA | MALAMBA MAWILI | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA | JASSON ALPHONCE MWAKITWANGE | BUNJU 'A' | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | AMOS MARWA NDEGE | NYUMBA | AMOS MARWA NDEGE | MSONGOLA-ILALA | 30/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NYERERE JACKSON MWERA | KIWANJA | NYERERE JACKSON MWERA | BUHONGWA-MWANZA | 25/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | BEATRICE FARES MLAY | NYUMBA | MACMILLAN SIFUEL KOWERO | BUSWELU,MAGAKA-MWANZA | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER NSHANA | BUNJU-KINONDONI | 26/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | 1.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 ,2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NAMBA 172590 KIWANJA NAMBA 399 KITALU 'L' | 1.SADIKI NTAHONDI MAPORO 2. DAVID ABEL MLAU | 1.CHARAMBE -MBAGALA , 2. MKURANG | 30/08/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0762260787/0714939933/0718038313/0743885084/0754497396
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

21693701

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua madhubuti zichukuliwe kupunguza ajali za barabarani

**WIMBI** la ajali za barabarani nchini limeendelea kuongezeka katika maeneo mbalimbali huku watu kadhaa wakipoteza maisha na wengine kujeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu.

Matukio hayo ya ajali yamekuwa kama jambo la kawaida kutokana na vyombo vya habari na vyombo vya usalama hususan polisi, kuripoti mara kwa mara. Mfano, jana watu 20 walifariki dunia na wengine 15 kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha magari mawili na trekta katika eneo la Mwakata, Msalala, Kahama mkoani Shinyanga barabara itokayo mji mdogo wa Isaka kwenda Kahama.

Ajali hiyo iliyotokea usiku wa kuamkia jana, ilihusisha gari aina ya Toyota IST lenye namba za usajili T 880 DUE, Hiace, T 350 BDX na lori aina ya Scania T 658 DUW, baada ya kugongana uso kwa uso. Tukio hilo ni mwendelezo wa ajali zinazoendelea kutokea na kusababisha watu kupoteza maisha huku ndani ya mwaka huu pekee, kumekuwa na ajali kadhaa ambazo zimegharimu maisha ya watu.

Ndani ya kipindi cha takriban mwezi mmoja, kuna ajali kadhaa zimetokea ikiwamo ile ya mkoani Mtwara iliyosababisha watu 13 wakiwamo wanafunzi wanane kufariki dunia papo hapo na wengine majeruhi wakiendelea kupatiwa matibabu. Julai 12, mwaka huu, pia watu wanane wakiwamo watano wa familia moja walipoteza maisha katika ajali iliyotokea Nyakahuri, Biharamulo mkoani Kagera baada ya gari walilokuwamo kugongana uso kwa uso na lori la mizigo.

Aidha, mwanzoni mwa Julai, mwaka huu, watu watano walipoteza maisha katika ajali iliyosababishwa na lori lenye shehena ya mahindi kufeli breki na kugonga basi dogo la abiria aina ya Toyota Coaster kwenye mteremko mkali wa barabara kuu ya Mbeya- Dar es Salaam.

Hizo ni ajali chache kati ya nyingi zilizotokea mwaka huu lakini Februari 14, mwaka huu, watu watano wakiwamo watatu wa familia moja, walifariki dunia eneo la Tura, Uyui mkoani Tabora. Ajali hiyo ilisababishwa na lori la mizigo na gari dogo aina ya Toyota RAV 4 lililokuwa likitoka Tabora kwenda Dar es Salaam.

Kama vile haitoshi, Machi 27, mwaka huu, watu saba walifariki dunia na wengine wanane kujeruhiwa baada ya lori la mizigo kugonga Bajaj katika eneo la Kidulya nje kidogo ya mji wa Bariadi mkoani Simiyu.

Sababu za kutokea kwa ajali hizo karibu zinafanana. Katika ajali ya jana, kwa mfano, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Leonard Nyandahu, alisema chanzo ni uzembe wa madereva wote ambao hawakuchukua tahadhari wakiwa katika vyombo hivyo.


Kamanda huyo alibainisha kuwa katika tukio hilo, kulitokea ajali mbili tofauti, ya kwanza ilihusisha trekta lililokuwa limesimama pembezoni mwa barabara bila kuwapo kwa viashiria kuonyesha kusimama, hivyo kusababisha Toyota IST kugonga kwa nyuma na kupata majeruhi.

Ajali ya pili, alisema ilihusisha Toyota Hiace iliyokuwa ikitokea Kahama kwenda Tinde wilayani Shinyanga, baada ya kugongana uso kwa uso na lori wakati ikijaribu kukwepa IST na trekta. Mbali na sababu za ajali ya jana, katika matukio ya nyuma imekuwa ikielezwa kuwa vyanzo vya ajali ni uzembe wa madereva, breki kufeli na mwendokasi wa madereva.

Kwa ujumla, ajali hizi sasa zimekithiri, hivyo hatua kali na za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kudhibiti ongezeko na kupotea kwa nguvu kazi ya taifa ambayo imekuwa ikiteketea kila uchao. Jambo moja kubwa linalotakiwa kuchukuliwa ni udhibiti wa vyombo vya moto viwapo barabarani na kwa kuanza kabisa kukagua magari yote pamoja na kutoa elimu ya usalama barabarani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kukubali matokeo kupewe nafasi baada ya uchaguzi

Na Beatrice Mosses

**MAJIRANI** na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kenya, wamemaliza uchaguzi mkuu unaotajwa na vyombo vingi vya habari kuwa ni wa amani, utulivu na hali ya usalama,

Imedhihirisha kwenye maeneo mengi nchini humo wakati wananchi wakitekeleza haki yao ya kidemokrasia, amani ilitawala. Sasa kinachosubiriwa ni matokeo ya uchaguzi huo na wapigakura wenyewe, pia nchi nyinginezo zikiwamo za ukanda wa Afrika Mashariki na marafiki wa nje na ndani ya Afrika.

Linalotumainiwa ni wagombea watakaoshindwa watakuwa na hekima na uvumilivu badala ya kutawaliwa na jazba, chuki na pengine tamaa ya kujipatia madaraka hata bila ya kibali cha sanduku la kura.

Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kenya inatajwa kuongoza kwa maelezo kuwa iko juu kiuchumi ikilinganishwa na mataifa mengine, hivyo matokeo ya uchaguzi huo ni muhimu yakapokelewa kwa amani na utulivu kwa kuwa ndiko kufanikisha, kuendelea na kutekelezwa kwa mipango iliyoko yenye lengo la kuimarisha mtangamano wa Afrika Mashariki kwenye kibiashara na uchumi.

Mchuano mkali unabaki kwa wagombea William Ruto na Raila Odinga, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu anayepeperusha bendera ya Muungano wa Azimio la Umoja, pia anaungwa mkono na Rais Kenyatta, na kwa upande wake mshindani wake ni Naibu Rais William Ruto, ambaye anagombea nafasi hiyo kwa tiketi ya Muungano wa Kenya Kwanza, lakini akiacha historia ya kukwaruzana na bosi wake Rais Kenyatta.

Wakati wa kampeni kali ya uchaguzi wagombea hao licha ya kushambuliana kwa maneno makali na kukosoana Odinga na Ruto pia wameripotiwa mara kadhaa na vyombo vya habari wakisisitiza amani ili kuiepusha Kenya kuingia kwenye machafuko ya uchaguzi wa 2007/2008.

Kuwepo kwa msisitizo huo waliouweka

> **Pamoja na kuchelewesha maendeleo kwa jamii na taifa, hivyo ni vyema kukubaliana na matokeo ili kuepusha machafuko na kulinda amani na maisha ya watu.**

unaotoa matumaini kwamba wanajitambua vyema kwenye ushindani wakiamini kuwa kuna kushinda na kushindwa, hivyo atakayeshindwa asitumie nafasi yake vibaya kwa kuhamasisha machafuko nchini humo.

Ni vyema nyakati za uchaguzi kila mmoja kuangalia mambo ambayo yamekuwa yakitajwa kuichafua Afrika kwa kuwa yamesababisha watu wengi kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu, kukosa makazi na mali zao kupotea.

Pamoja na kuchelewesha maendeleo kwa jamii na taifa, hivyo ni vyema kukubaliana na matokeo ili kuepusha machafuko na kulinda amani na maisha ya watu.

Katika machafuko ambayo yanatajwa kusababishwa na kuenezwa kwa taarifa za madai ya udanganyifu katika uchaguzi wa rais wa Desemba 2007, Kenya iliingia kwenye vurumai zilizochochea kuzuka kwa vurugu zilizosababisha Wakenya zaidi ya 1,500 kuuawa na wengine wengi kuwa wakimbizi wa ndani.

Iwapo machafuko yataibuka nchini humo kutokana na matokeo ya uchafuzi, ni wazi kuwa miongoni mwa nchi hizo wanachama zitalazimika kupokea wakimbizi, hivyo zile fursa za ushirikiano wa kibiashara katika mazingira hayo zitakuwa zimelegea au kufungwa kwa muda usiojulikana, ndiyo maana inasisitizwa kuwa matokeo yapokelewe kwa utulivu na uvumilivu.

Bado zipo juhudi za kuwa na sarafu moja na soko la pamoja la Afrika Mashariki, kuna ujenzi wa miundombinu ya kuimarisha mtangamano na mengine mengi.

Ikumbukwe mara nyingi wanaokufa ama kujeruhiwa kwenye machafuko ya kisiasa wengi ni wananchi wa hali ya kipato cha kati na cha chini, kwa hiyo ni vyema raia nao wakaepuka kutumika na wanasiasa wanaotaka kama itakuwa na jambo ambalo litabainika kuwa limefanywa isivyo lifikishwe kwenye vyombo vya sheria ili kuipata nafasi kufuata mkondo wake badala ya kufanya vurugu.




Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa Benki ya NMB, Isaac Masusu (kushoto) na Meneja wa Benki hiyo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola wakifurahia tuzo ya taasisi ya fedha kinara katika maonyesho ya Nanenane, yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asilimia 60 wasiojua kusoma na kuandika wana uoni hafifu

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET) imesema asilimia 60 ya wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika wana matatizo ya uoni.

Mkurugenzi Mkuu wa TET, Aneth Komba, alisema hayo jana Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli za taasisi hiyo na mwelekeo wa utekelezaji wake kwa mwaka fedha 2022/23.

Alisema matokeo hayo ni kutokana na utafiti uliofanyika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Western Norway.

Dk. Komba alisema utafiti huo pia ulibaini walimu hawana ujuzi wa kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi, hivyo kushindwa kuwapatia watoto hao afua wanazostahiki hali inayopelekea watoto hao kumaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika.

Alisema kutokana na matokeo hayo, serikali ilitenga Sh. milioni 82.64 kwa ajili ya kuandaa moduli za kuwafundisha walimu, ili waongeze umahiri wa kuwabaini wanafunzi wenye changamoto zinazowarudisha nyuma wakati wa kujifunza katika ngazi ya elimu ya msingi hadi sekondari.

"Kupitia utafiti huo, TET inaandaa moduli za kuwawezesha walimu hao kuwa na umahiri wa kuwabaini watoto hao na kuwapa msaada stahiki, ili kufanya vizuri kwenye masomo yao," alisema Mkurugenzi huyo.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Aga Khan, Aga Khan Foundation na Ed-Tech HUB itafanya utafiti wenye lengo la kubaini teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) iliyo nafuu na endelevu itakayofaa kutumika kutoa mafunzo ya walimu kazini.

Alisema Sh. milioni 850 zimetengwa kugharamia utafiti huo wenye lengo la kuboresha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya elimu ya msingi kwa shule zilizopo vijijini.

Dk. Komba alisema mwaka 2020/21 serikali ilitoa Sh. milioni 1.24 iliyosadia utoaji mafunzo kwa walimu 4,627 wa elimu ya awali, msingi na sekondari.

"Walimu hawa wamepatiwa mafunzo ya utekelezaji wa mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri. Jumla ya wasimamizi 1,200 wa utekelezaji wa mtaala walipatiwa mafunzo wakiwemo wadhibiti ubora wa shule na maofisa elimu wilaya na kata," alifafanua.

Dk. Komba aliongeza kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 Sh. bilioni 1.4 zimetengwa kuendelea na mafunzo kazini kwa walimu na wasimamizi wa utekelezaji wa mitaala 8,500.

Pia alisema katika kuhakikisha vitabu wanavyotoa vinatumika katika malengo kusudiwa, wanafanya ufuatiliaji katika shule huku wakigundua kuwa baadhi ya shule wanafungia vitabu hivyo ili visiharibike .

"Tunapofuatilia tunagundua kuwa shule nyingine vitabu vimefika lakini kwa bahati mbaya sana walimu wanavifungia kwenye makabati na ukiwauliza ni kwa nini wanasema hawataki vitabu viharibike," alisema.

Pia alisema wameandaa mfumo wa kidijitali wa kuwasiliana na shule moja kwa moja kwa kutumia simu janja, ili kupata taarifa kutoka kwa walimu ikiwa wamepata vitabu au la.

"Serikali imetenga Sh. bilioni 1.7 zitakazotumika katika mchakato kukusanya maoni kuhusu rasimu za mitaala pendekezwa na kuandaa vifaa vingine vya utekelezaji wa mitaala ikiwamo mihtasari na kutoa mafunzo.

"Katika kufanya kazi ya mapitio ya mitaala, suala la kukusanya maoni kutoka kwa wadau ni endelevu.Taasisi kwa kushirikiana na kamati ya kitaifa ya mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda, inaendelea kukutana na makundi mbalimbali ya wadau," alisema.

**Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR) na Loyce Cyriacus (SJMC)**

# NHC kupoteza bil. 6/- wadaiwa sugu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

DENI la Shilingi bilioni sita linalodai Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) wateja wake, limebainika halitalipwa kutokana na wadaiwa kufariki na kampuni kufilisika.

Aidha, katika mwaka 2022/23, Shirika hilo litatumia Sh. bilioni 413.7 kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwamo ujenzi wa nyumba 5,000 za gharama ya kati nchini 'Samia Housing Scheme (SHS)'.

Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika hilo, Muungano Saguya, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapo, alisema hadi Desemba mwaka 2021 kulikuwa na deni la Sh. bilioni 26 wanalodaiwa wadaiwa sugu wa NHC.

"Ni fedha nyingi ambazo zingepatikana shirika lingewekeza kwenye miradi mingine, tulifanya operesheni ya kuwatoa wapangaji na wanaodaiwa sana, lakini tulifanya operesheni ya kufuatilia nyumba kwa nyumba na tulipitia upya madeni haya kuangalia nani ni nani na anadaiwa, yupo wapi na kwanini."

"Kuna madeni yanayofika Shilingi bilioni sita yanasubiri kupata kibali cha Bodi ya Wakurugenzi ili kufutwa, haya ni madeni ambayo hayakusanyiki ama watu walishafariki, ama kampuni zilishafilisika au hazipo tena, kwa hiyo kuna changamoto nyingi sio rahisi kueleza kwa takwimu sahihi," alisema.

Alitoa wito kwa wapangaji na wadaiwa sugu wa kodi ya pango kuhakikisha wanalipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa kwa kuwa shirika kuanzia sasa litakusanya kwa asilimia 100.

**MRADI WA MOROCCO**

Saguya alisema Mradi wa 'Morocco Square' unatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu sambamba na miradi ya Kawe 711 na Golden Premier Residence (GPR), iliyopo Kawe, jijini Dar es Salaam.

**MRADI WA SAMIA**

Alisema mradi huo unakusudia kuenzi kazi nzuri anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan asilimia 50 ya nyumba hizo zitajengwa Dar es Salaam, Dodoma asilimia 20 na mikoa mingine asilimia 30.

"Nyumba hizi zitaanza kujengwa mwezi Septemba eneo la Kawe Dar es Salaam (nyumba 500) na Medeli, jijini Dodoma (nyumba 100). Mradi huu utakaotekelezwa kwa awamu utagharimu Sh. bilioni 466," alisema.

Alisema mradi utatoa ajira 26,400 kwa Watanzania na utatengeneza mapato ya kodi mbalimbali na kuongeza maisha bora kwa wananchi.

"Taarifa ya UN Habitat ya hali ya idadi ya watu inasema kuwa asilimia 50 ya watu waliishi mijini mwaka 2020 na ifikapo mwaka 2050 idadi itakuwa asilimia 70 na Tanzania itakuwa na watu milioni 135 na mwaka 2100 itakuwa na watu milioni 286 na kuwa nchi ya tisa duniani. Hii inahitaji mipango madhubuti ya kupanga miji na upatikanaji wa nyumba," alisema.

**MTAJI WA SHIRIKA**

Shirika lina mtaji wa Sh. trilioni 5.04 hivi sasa unaotokana na rasilimali ya majengo yake 2,650 yenye nyumba 18,654 zilizoko kwenye mikoa mbalimbali nchini.

**SERA YA UBIA**

Alisema Septemba, mwaka huu, shirika linatarajia kuzindua utekelezaji wa Sera ya Ubia itakayoruhusu sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji wa maeneo ya NHC.

"Sera hii ina lengo la kuharakisha uendelezaji wa maeneo yaliyo wazi katikati ya miji yetu kwa kujenga nyumba za vitega uchumi na hivyo kuliongezea shirika na nchi mapato makubwa," alisema.


**Amicus Attorneys**
Advocates, Notaries Public & Commissioners for Oaths

## NOTICE OF OUTRIGHT PURCHASE

A. Bids are invited for the outright purchase of the following properties, to wit: -

1. A storey building located at an upmarket area in Kawe Low Density Area, Plot No. 448, Dar es Salaam City in the name of Mukesh Vrajlal Kanabar, P.O. Box 2915, Dar es Salaam; and

2. An apartment in **Kariakoo Area, Plot No. 18, Block 26, Ilala Municipality** in the name of AK'S Limited, P.O. Box 2915, Dar es Salaam.

B. Bidders are invited to purchase the above-mentioned properties under receivership. Interested bidders should submit their bids for the purchase of the properties to the Receiver/Manager so as to reach the Receiver/Manager at the address below within 30 days from the date of this Notice. No bid fee is required.

C. Bidders may contact the Receiver/Manager to obtain a copy of the latest valuation report of the properties.

D. Those interested to view the properties should contact the Receiver/Manager during office hours. E. The Receiver/Manager is not obliged to accept the highest or any bid at all.

F. Bids in sealed envelopes indicating clearly the particulars of the property or properties being tendered for should be addressed to the Receiver/Manager at the following address: -

**Dr. Abduel G. Kitururu (PhD) Receiver /Manager**
**C/O Amicus Attorneys**
**IPS Building, 7th Floor - Left Wing**
**Samora Avenue/Azikiwe Street**
**P.O. Box 7219**
**Dar es Salaam.**
**Mob. 0715707170; 0762707170; 0784707170**
**Tel. 0222129160; Fax 0222129160.**

21698I902

# DAWASA yawa mbogo uharibifu miundombinu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imewataka wakazi wa Mtaa wa Ulongoni B na Dar es Salaam kwa ujumla kuwafichua wanaohujumu miundombinu ya majisafi hususani mita na koki za maji.

Ofisa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka hiyo, Felister Mrema, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki katika kikao cha wananchi na DAWASA kilichoandaliwa kwa lengo la kuwaelimisha wateja kuhusu huduma za mamlaka hiyo.

Aliongeza kuwa serikali kupitia mamlaka inatumia gharama kubwa kutekeleza miradi ya kufikisha huduma ya majisafi kwa wateja ili kila mwananchi apate huduma ipasavyo.

"Wananchi mnatakiwa kuwa walinzi wazuri wa miundombinu ya maji kwa kuepuka kuhujumu vifaa vya maji na kutoa taarifa kwa watu wanaojihusisha na tabia hiyo," alisema na kubainisha kuwa tabia hiyo inarudisha nyuma jitihada za serikali kufikisha huduma kwa wateja.

Mrema aliwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kukagua mita zao za maji kila wakati kwa lengo la kubaini uvujaji na kutoa taarifa ili kuokoa upotevu wa maji vilevile kujua kiasi cha maji walichotumia kwa mwezi huo.

"Ukaguzi wa mita za maji mara kwa mara unasaidia kumpa mteja uhakika wa maji yanayotumika hivyo jengeni utamaduni wa kuzikagua mara kwa mara," alisema.

Pia aliwataka wananchi wa Ulongoni B kuchangamkia fursa ya maunganisho ya maji kwenye mitaa yao kwa kuwa mamlaka imeshasogeza miundombinu ya maji karibu na makazi yao.

"Kwa sasa serikali imewapa wananchi unafuu wa kupata huduma kwa njia ya mkopo, hivyo wananchi mnakaribishwa ofisini ili kupata utaratibu wa kupata mkopo," alisema na kuwasisitiza watendaji na wenyeviti wa Ulongoni kuwahamasisha wakazi kujitokeza kupata huduma ya majisafi na kuachana na matumizi ya maji ya chumvi.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Ulongoni B, Mohammed Mzara, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kuepuka kuiba vifaa na miundombinu ya maji hali inayofifisha jitihada za serikali.

Aliongeza pia kuwa mamlaka inafanya kila jitihada kuhakikisha huduma inafika na inakua imara kwa wateja wote.

"Uongozi wa serikali ya mtaa unajitahidi kuhakikisha unadhibiti watu wote wanaojihusisha na uhalifu wa miundombinu ya maji, tutaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuacha tabia hii ya wizi wa miundombinu," alisema.

Mkazi wa Ulongoni B, Ibrahim Katungi, alishauri mamlaka kuangalia njia nyingine mbadala ya kufunga mita za maji sehemu ambayo haitaweza kuguswa na wahalifu ili kuepuka wizi huo.

Alisema pia kuwa wananchi wanapaswa kuwa walinzi namba moja wa mita hizo kwa kuzijengea kisanduku ili kuepuka wizi.



Viongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), wakiwa katika mkutano kwa njia ya mtandao na maofisa wa Chuo cha Ufundi Zibo (ZBVI) cha nchini China, jijini Dar es Salaam jana. Chuo cha ZBVI kitatoa utaalamu kwenye mafunzo ya ufundi stadi kwa wakufunzi wa NIT ambao baada ya hapo watatoa ujuzi huo kwa wanafunzi wanaosomea uhandisi wa magari katika chuo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwanadiaspora ahimiza kusaidia wenye uhitaji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Loveness Foundation (LF) ilyoanzishwa mwaka jana huko Marekani kwa ajili ya kuboresha maisha ya jamii ya Waafrika waliosahaulika wanaoishi maeneo ya vijijini na Marekani, imehimiza kutoa msaada kwa makundi hayo.

Rais na Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Loveness Mamuya, alisema juzi kuwa wanafanya kazi kupitia mpango mkakati wake wa miaka mitano (2022-2026) unaojumuisha na kuelezea dhima, maono, vipaumbele, majukumu, malengo na misingi ya utendaji wake.

Alisema mpango huo unaanza na uchambuzi wa ukweli unaojiri Afrika na mazingira yake yanayoshawishi mipango mbadala.

Alisema mpango huo pia umejikita katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), akisisitiza lengo lao ni kuwawezesha na kuwashawishi wanawake, wazee, watoto na vijana kuinuka kiuchumi.

"Taasisi ya Loveness nimeianzisha kwa malengo mahsusi ya kuwasaidia watu wote au jamii ya watu wenye uhitaji kupitia makundi yao maalumu.

"Kupitia taasisi, ninawasaidia watu wa makundi hayo maalum si kwa sababu ya vile walivyo au kwa sababu ya kile wanachokifanya, hapana. Ninafanya hivyo kwa sababu hivyo ndivyo tunavyotakiwa kuwasaidia watu wenye mahitaji," alisema.

Loveness, Mtanzania anayeishi Marekani, anasema lengo lingine la taasisi yake ni kuboresha maisha ya watu hao kwa kuangazia uzalishaji wa vipato vyao, afya, elimu, mazingira safi na haki jamii.

Kupitia msukumo wake na kuvutiwa binafsi na masuala ya afya na ujasiriamali, Loveness amejikita zaidi kusaidia mashirika na vikundi vidogo na vya kati vya Tanzania na nje ya nchi.

Mwana diaspora huyo pia anaamini kwamba afya ni jambo muhimu kwa ukuaji, maendeleo na ushiriki wa mambo mbalimbali yanayojiri duniani na kupitia kujifunza ujuzi kwa ajili ya kutafuta njia za kutimiza malengo yao.

# Wanafunzi NIT kunolewa teknolojia ya magari, mitambo

**Na Prosper Makene**

WANAFUNZI wa stashahada ya mafunzo ya uhandisi wa magari (Automobile Engineering) katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), wataanza kufundishwa teknolojia za magari na mitambo ya kichina kuanzia mwaka huu wa masomo.

Hatua hiyo imekuja baada ya chuo hicho kuingia makubaliano ya ushirikiano na Chuo cha Ufundi Zibo (ZBVI) kutoka Jimbo la Shandong, China kwenye eneo la ufundi stadi.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, ZBVI itatoa utaalamu kwenye mafunzo ya ufundi stadi kwa wakufunzi wa NIT ambao baada ya hapo watatoa ujuzi huo kwa wanafunzi wanaosomea uhandisi wa magari katika chuo hicho.

Jijini Dar es Salaam juzi baada ya kuingia katika makubaliano hayo, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa alisema:

"Kupitia makubaliano haya, Chuo cha Ufundi cha Zibo kitatoa mafunzo kwa wakufunzi wetu kwenye eneo la uhandisi wa magari na mitambo mbalimbali ya Kichina.

"Chuo chetu kimefarijika sana na makubaliano haya ya ushirikiano, kwa kuwa itatusaidia kuboresha mtaala wetu wa uhandisi wa magari."

Prof. Mganilwa alisema katika mwaka wa masomo 2022/23, baadhi ya wakufunzi wa uhandisi wa magari katika chuo hicho watapata fursa ya kujifunza teknolojia ya magari ya Kichina ili kuwafundisha wanafunzi wao.

"Ushirikiano huu siyo tu utatoa fursa kwa wanafunzi wetu kujifunza teknolojia za magari na mitambo ya Kichina bali pia utachangia katika kuimarisha zaidi uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na China," alisema.

Aliongeza kuwa makubaliano hayo ya ushirikiano yatatoa fursa kwa wanafunzi wa Kitanzania kwenda China kujifunza teknolojia za utengenezaji magari kwa msaada wa kampuni mbalimbali za nchi hiyo.

Alibainisha kuwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaonunua magari na mashine kutoka China hawatakuwa na wasiwasi tena baada ya kuanza kwa mpango huo.

Alisema kuwa katika kila muhula, wanafunzi wanaosoma stashahada hiyo ya ufundi wa magari watakaochaguliwa kulingana na ufaulu wao, watafundishwa moduli moja ya teknolojia ya magari ya Kichina.

"Nafasi ya China katika uchumi wa dunia imekuwa imara sana kiasi kwamba wanafunzi wetu watafaidika kwa kujifunza teknolojia za magari ya Kichina, ni matumaini yangu mhitimu wa uhandisi wa magari atatumia fursa zote za soko la China na Afrika," Prof. Mganilwa alisema.

Mkataba huo wa mashirikiano umehusisha pia kampuni zingine mbili kutoka China ambazo ni Tianjin Zhongwu Education Technology Co. Ltd na Taasisi ya Mafunzo ya Mafuta na Gesi ya Sunmaker.

Makubaliano hayo ni matokeo ya Mkutano wa Beijing na Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika ambapo pamoja na mambo mengine wajumbe wake waliridhia uanzishwaji wa karakana 10 barani Afrika ili kuweza kusambaza teknolojia za magari na mitambo ya Kichina.

Ni hatua hiyo iliyosababisha taasisi nne za NIT, ZBVI, Tianjin Zhongwu Education Technology Co. Ltd pamoja na Taasisi ya Mafunzo ya Mafuta na Gesi ya Sunmaker kukubaliana kuanzisha karakana za Luban nchini ili kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana wa Kitanzania.

Akihutubia katika Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika lililofanyika jijini Beijing Septemba, 2018, Rais wa China, Xi Jinping alisema:

"Tutazindua mpango wa kujenga uwezo. China itashiriki zaidi shughuli zake za maendeleo na Afrika na kusaidia ushirikiano na Afrika katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; tutaanzisha karakana 10 za Luban barani Afrika ili kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana wa Afrika."

## Bilioni 1.6/- kupeleka umeme Manispaa Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani Kahama limetenga Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya kupeleka umeme katika kata zisizokuwa na huduma hiyo Halmashauri ya Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama ili kurahisisha viwanda kufanyakazi.

Pia, limetenga zaidi ya Sh. bilioni 700 za uboreshaji wa upatikanaji wa huduma hiyo katika kata za Malunga, Bukondamoyo, Kagongwa, Malunga, Nyihogo, Mtaa wa Namanga CDT na fedha hizo zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, Jimmy Monyo, aliyabainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Manispaa ya Kahama cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 kilichojadili masuala mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo afya, maji, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema, kila mwaka wanapokea fedha za kupeleka huduma ya nishati ya umeme katika vijiji na kata zisizokuwa na huduma na mwaka huu wa fedha 2022/2023 wamepokea Sh. bilioni 1.6 za kupeleka nishati kata za Halmashauri ya Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama.

Aidha, Monyo alitaja kata za halmashauri hiyo zitakazopata huduma ni za Nyasubi, Mwendakulima, Busoka, Mwime-Zongomela, Nyambula, Mhongolo, Kitwana na Nyambula pamoja na kata 38 za Halmashauri ya Ushetu na Msalala na lengo ni kufufua viwanda vidogo vilivyoko.

"Asilimia 80 ya vibarua watakaofanyakazi wakati wa utekelezaji wa miradi hii ni wale walioko katika vijiji na kata husika, hivyo zile zitakazohitaji utaalamu zaidi watatoka kwetu TANESCO...Niwaombe madiwani katika vikao vyenu katani mlifikishe jambo hili," alisema Monyo.

Naye Diwani wa Mondo, Kija Peja alisema, wakati wa kuunganishiwa huduma hiyo kupitia mradi wa REA, wananchi waliunganishiwa kwa Sh. 27,000 na vijiji vyote vilipata umeme, lakini kwa sasa gharama zimeongezeka hadi Sh. 300,000 fedha ambazo wenye uwezo wa chini hawawezi kuimudu.

Diwani wa Busoka, Julius Mlale alisema, maeneo mengi katika kaya yake hakuna umeme ikiwamo ofisi yake mpya ya kata na mradi utakapoanza watoe kipaumbele taasisi za elimu na afya na kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi kutoka gharama ya Sh. 27,000 mpaka mpya.

# Kibiti wahakikishiwa mradi maji, kuunganishwa umeme TANESCO

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

MENEJA wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Kibiti, Pascal Kibangule, amesema wanatarajia kuunganisha mradi wa maji Miwaga Ngulakula na umeme wa TANESCO ili kuondokana na matumizi ya jenereta ambalo limekuwa kikwazo cha upatikanaji maji kwa wananchi.

Kibangule aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu walivyojipanga kutatua kikwazo cha upatikanaji maji ya uhakika kwa wakazi wa Miwaga na Ngulakula, kata ya Dimani, wilayani Kibiti.

Alisema tangu mradi huo ulipokamilika 2021 na kukabidhiwa Bodi ya Maji ya Kata ya Dimani, yalikwama kutoka kutokana na kutofanyika kwa matengenezo na kusababisha yasitoke.

"Utatuzi wa kudumu wa maji katika maeneo hayo ni kutoa mfumo wa kutumia dizeli na kuunganisha umeme na tayari TANESCO wameshapata mkandarasi atakayefanya hivyo kupunguza gharama za uendeshaji hii hasa ni kutokana na kupanda gharama za dizeli," alisema Kibangule.

Hata hivyo, meneja huyo anaeleza kuwa baada ya kubaini kero ya ukosefu wa maji kwenye vijiji hivyo RUWASA imelazimika kuingilia kati na kufanya matengenezo ili wananchi hao wapate maji.

Hivi karibuni, wakazi wa vijiji vya Miwaga na Ngulakula wamelalamikia uwapo wa mradi wa maji ambao haujatatua kero yao ya muda mrefu kutokana na kutoka kwa kusuasua na kuwasababishia kutumia ya kisima ambayo yanapatikana mbali na makazi yao.

Ally Kambangwa, mkazi wa Ngulakula alisema hali ya maji imeendelea kuwa ngumu pamoja na kuwapo mradi huo wanaendelea kufuata maji kilomita mbili na wakati mwingine kununua maji dumu la lita 20 kwa Sh. 800.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilimbili, Jamal Matimbwa, alikiri kuwapo kwa kero hiyo ambayo inasababisha baadhi ya shughuli za maendeleo kusimama na wananchi kutumia muda mwingi kufuata maji.



Mgombea wa ubunge wa Afrika Mashariki kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Queen Lugembe (kushoto), akirudisha fomu kwa Naibu Mkurugenzi Mipango na Chaguzi wa chama hicho, Yusuph Mbungiro, katika ofisi kuu za CUF Buguruni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Singida kunufaika miradi sita ya maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida, umepata zaidi ya Shilingi bilioni nne fedha za UVIKO-19 kwa ajili ya kujenga miradi tisa ya maji mkoani hapo.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Singida, Lucas Saidi, akizungumza juzi baada ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, kuweka jiwe la msingi mradi wa maji ya bomba wa Rafiki-Ikungi, alisema miradi yote hiyo utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85.

Said alisema kati ya miradi hiyo, sita inatekelezwa vijijini kwa gharama ya Sh. bilioni 2.7 na mitatu mijini katika wilaya za Iramba, Manyoni na Singida Mjini kwa Sh. bilioni 1.28.

"Mradi wa Ikungi ambao unajengwa kwa Sh. bilioni 548 utakapokamilika utahudumia zaidi ya wananchi 7,000 ambapo kutakuwa na vituo 11 vya maji na wananchi watakuwa wakijiunganishia maji wenyewe majumbani mwao," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Muro, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kususia miradi ya maji inayojengwa na serikali kwa mamilioni ya fedha kwa kuendelea kunywa maji ya mabondeni, visima na mito ambayo sio salama kwa afya zao.

"Mradi huu umekamilika, ile tabia ya kwenda kunywa maji bondeni au mtoni kwa kisingizio mumeyazoea yana ladha nzuri iishe, tunywe maji ya bomba ili afya zetu ziwe nzuri, tuachane na maji ya visima," alisema.

Muro alisema hakuna sababu kwa wananchi kususia miradi ya maji kwa kuogopa kuchangia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo kwa kuwa serikali inawapenda wananchi wake na inataka kuhakikisha dhamira ya kumtua mama ndoo kichwani ambayo imekuwa ikisisitizwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inatimia.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutafanya upatikanaji wa huduma za maji katika Wilaya ya Ikungi kufikia asilimia 57.3 na kwamba malengo ya serikali ni kuhakikisha kiwango cha upatikanaji wa maji kinafikia asilimia 60 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema serikali wilayani Ikungi imeshapitisha kwenye vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Wilaya (DCC), mpango wa uboreshaji wa usambazaji wa maji katika tarafa ya Ikungi na maeneo mengine na Ikungi sasa itaanza kuhudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA).

Kwa upande wake, Kaimu Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Ikungi, Mhandisi Michael Ndunguru, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupunguza maambukizi ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa majisafi na salama na kusaidia wananchi kufanya shughuli za kiuchumi na kuondokana na kero ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

# Wenyeviti serikali mitaa lawamani migogoro ardhi

**Na Devota Mwachang'a**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema mojawapo ya sababu kubwa za migogoro ya ardhi nchini ni wenyeviti wa vijiji na mitaa kuwa vinara katika uuzaji ardhi kiholela kinyume na sheria.

Alisema kutofuata sheria za uuzwaji wa ardhi kumechochea ongezeko la migogoro hiyo na Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa migogoro mingi zaidi ikifuatiwa Dodoma na Mwanza.

"Wenyeviti wa vijiji na mitaa kwenye maeneo ya mipango miji hawana mamlaka ya kugawa ardhi, hata kama wanahisi yametelekezwa na kuwa vichaka. Wasiendelee kuwa sehemu ya migogoro ambayo inakwamisha shughuli za maendeleo katika mikoa yao," alisema Mabula.

Alibainisha hayo alipokuwa akiongea na waandishi wa habari baada ya kusikiliza kero za migogoro ya ardhi toka kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Aliwasihi wananchi wanaohitaji kununua ardhi wafike kwenye ofisi za halmashauri husika kuonana na wataalamu ili kujiridhihisha na kupata idhini kama muuzaji anamiliki eneo hilo kihalali.

Vilevile, ametoa wito kwa wamiliki wa ardhi kuendeleza maeneo yao kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ili kutovutia wenyeviti wa vijiji kugawa maeneo hayo kiholela.

"Wamiliki waendeleze maeneo yao wasiyaache kuwa kama vichaka, kadri wanavyochelewa kufanya hivyo ndivyo wavyozidi kuyafanya yaonekane kama yametelekezwa hayana wamiliki hali," alisisitiza.

Alifafanua kuwa kisheria mwenye eneo lake kama ameshindwa kuliendeleza halmashauri lazima impe onyo na baadaye apewe tangazo la kumwondoa, lakini kama hajapewa ilani na mamlaka husika yupo salama, tatizo ni kuwa katika maeneo mengi watumishi wa ardhi hawafuati sheria.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi wamemshukuru waziri kufika na kusikiliza kero zao pia kwa hatua ya kuweka dawati la utatuzi wa migogoro.

Abdallah Chande, mkazi wa Manispaa ya Ubungo alisema: "Ukosefu wa nyaraka halali za umiliki wa ardhi ndiyo tatizo kubwa kwa wananchi wengi, pia viongozi wa vijiji hawatunzi nakala za nyaraka hizo. Hapa Ubungo kuna kesi ya wananchi kuidai fidia serikali, baada ya kuchukua eneo la kujenga kituo cha afya."

Mwanahamisi Yunusi, kwa upande wake aliiomba serikali kupitia makamishna wa ardhi kutembelea maeneo yenye migogoro badala ya kukaa ofisini wakisubiri kesi ziwafikie. "Eneo letu limevamiwa na watu wameanza kujenga majengo. Namwomba Waziri aingilie kati kumwondoa mvamizi katika eneo langu Goba Block ambapo nimehangaika katika ngazi mbalimbali za kijiji bila kupata msaada wowote."

Serikali ilisema kwamba itashughukikia utatuzi wa migogoro ya ardhi nchi nzima kwa kuunda dawati maalumu kila eneo na kutembelea wananchi kusikiliza kero zao ili kumaliza migogoro isiyo ya lazima.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akikabidhi zana ya kilimo mahususi kwa uvunaji wa mpunga kwa mmoja wa wateja wa benki hiyo, ambaye ni mkulima, Stephano Msigwa, kwenye Maonyesho ya Kilimo Nanenane katika Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yaibuka kinara tuzo taasisi za fedha

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imekamilisha ushiriki maonesho ya Nanenane kwa kuibuka kinara wa tuzo ya kundi la taasisi za fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alikabidhiwa tuzo na waandaaji wa maonesho hayo ikiwa ni ishara ya kutambua umahiri, mchango na ushiriki wa taasisi hiyo katika kufanikisha maonesho hayo ya wadau wa kilimo.

"Tuzo hii ni uthibitisho kuwa jitihada kubwa zinazofanywa na Benki ya NBC kuhakikisha tunakuwa karibu zaidi na wadau wa kilimo kwa namna mbalimbali ikiwamo utoaji wa huduma zetu hadi ushiriki wetu," alisema.

Akizungumzia ushiriki wa benki hiyo kwenye maonesho hayo, alisema ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo kukuza sekta ya kilimo nchini kupitia mpango wake mahususi unaofahamika kama 'NBC Shambani' ukihusisha mnyororo wote wa sekta ya kilimo kuanzia kwa mkulima, mchakataji wa mazao ya kilimo hadi msambazaji kuendelea kujiweka karibu zaidi na wadau wa sekta hiyo muhimu.

"Kupitia maonesho haya tumepata fursa ya kutangaza huduma zetu zinazohusiana na sekta nzima ya kilimo pamoja na kupokea mrejesho wa huduma hizo kutoka kwa wakulima na wadau wengine wengi wakiwamo viongozi mbalimbali waliotembelea banda letu wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya, wabunge, mawaziri na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Dk. Tulia Ackson," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na wakulima kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema tangu kuanza kwa maonesho hayo hadi kukamilika wamefanikiwa kukutana na wadau mbalimbali wa sekta hiyo muhimu huku wengi wakionesha kuvutiwa zaidi na huduma ya Bima ya Kilimo inayotolewa na benki hiyo.

"Bima hii inalenga kuwalinda wakulima, wavuvi na wafugaji nchini dhidi ya hasara pindi wanapopata majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri uzalishaji wao. Tunashukuru kuona kupitia maonesho haya wadau wameonesha kuipokea vizuri zaidi hali ambayo inazidi kutupa nguvu zaidi na ari ya kuendelea kubuni huduma mpya. Tunaamini kwamba kupitia maoni tuliyoyapata kutoka kwa wadau waliotutembelea siku chache hizi yatatuwezesha kubuni huduma bora zaidi zinazoendana na mahitaji ya wadau husika," aliahidi.

# Chalamila awaonya wananchi kuchokoza polisi

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amewataka wananchi kutii sheria bila shuruti na kuacha kupambana na Jeshi la Polisi linapokuwa kazini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Chalamila katika Kata ya Nyanga, Manispaa ya Bukoba kwenye kilele cha maonesho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane.

Chalamila alisema hakuna sababu ya mwananchi kuchukua mawe na kuwarushia polisi kwa kuwa wao wana mafunzo na wanajua namna ya kulinda taifa lao.

Alisema wapo wananchi wilayani Kyerwa ambao walichukuliwa magunia yao ya kahawa na kutaka kuyavusha kwenda nchi jirani kwa lengo la kuyauza na walipokamatwa wakajaribu kupambana na Jeshi la Polisi.

"Mimi nawashukuru askari wa Jeshi la Polisi kwa kuwa wapole, lakini sina hakika upole huo utakuwa mpaka lini, sababu utakuta mwananchi anakwenda hadi polisi anamrushia mawe polisi," alisema Chalamila.

Alisema, hakuna sababu ya kushika mawe na kumrushia polisi, amani ilindwe na isichezewe, serikali inalenga kuwa na wawekezaji ili wananchi wake wanufaike.

Aliongeza kuwa kuendelea kutorosha kahawa haisaidii mwananchi na kunasababisha kupoteza mapato ya serikali.

Alisema sekta ya kilimo katika mkoa huo ni nguzo kubwa ya kuinua uchumi na inaendelea kuchangia sehemu ya pato la nchi.

Alisema serikali inatambua mchango wa sekta ya kilimo na kwa kuona hilo imeongeza bajeti katika eneo hilo kutoka Sh. bilioni 300 hadi Sh. bilioni 800 kwa mwaka 2022/2023.

UCHAGUZI KENYA
Wakenya wamemaliza kazi sasa ni zamu ya shujaa atakayevikwa taji
Ukurasa 13



Ukurasa 14





**MATOKEO UCHAGUZI KENYA**
**Ni zamu ya kumsubiri anayepindua meza kibabe, kambi ya Ruto, Raila**

# Kenya wanapomaliza jambo lao kwa amani

**Na Mwandishi Wetu**



Mamia ya wapigakura kwenye misururu wakiwa katika kituo cha kupigia kura nchini Kenya. **PICHA:AFP.**

KULIPOPAMBAZUKA saa 12 alfajiri, Wakenya walifanya uamuzi wa kumchagua mrithi wa Rais Uhuru Kenyatta, katika uchaguzi unaotajwa na vyombo vya habari kuwa ni wa amani na utulivu.

Wakati wapigakura wanakimbilia vituoni licha ya kusongwa na gharama kubwa za maisha, ukosefu wa ajira na ufisadi, masuala yaliyotawala kampeni za wagombea wakuu wa urais Raila Odinga na William Ruto, kilichojiri ni kuchaguana kwa amani.

Wagombea wakuu hao, wanashindana kumrithi Uhuru Kenyatta, ambaye amemaliza miaka 10, akiiongoza Kenya kuanzia Aprili 2013. Katiba ya Kenya inampa rais mihula miwili ya uongozi kwa utaratibu wa miaka mitano mara mbili.

Taarifa ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC) inasema wagombea 16,000 wanawania nyadhifa 1,879 za kuchaguliwa, zikiwemo za rais, wabunge wa Seneti au Bunge Dogo na Bunge la Kitaifa, magavana na wawakilishi wa bunge la kaunti. Wakati wapigakura waliojisajili ni milioni 22.

**ILI KUSHINDA**

Matokeo rasmi ya uchaguzi wa jana yanatangazwa ndani ya wiki moja. Katika taifa hilo lenye watu milioni 53, wapiga kura zaidi ya milioni 22 waliojiandikisha, macho na masikio yao yanaelekezwa kwa Naibu Rais Ruto anayegombea kupitia Muungano wa Kenya Kwanza na Raila Odinga, mpinzani anayepeperusha bendera ya Muungano wa Azimio la Umoja.

Wagombea wengine ni George Wajackoyah wa Chama cha Roots na David Mwaure wa Chama cha Agano, ambao wanaweza kuitwa wasindikizaji.

Ili Ruto au Raila ama Wajackoyah au Mwaure mmoja wao atangazwe mshindi anahitaji kupata zaidi ya nusu ya kura zote. Ina maanisha kama zitapigwa zote milioni 22 ni lazima kupata nusu yake.

Aidha, wagombea hao wa urais pamoja na kuhitaji zaidi ya nusu ya kura zote wanatakiwa kushinda zaidi ya asilimia 25 ya kura katika zaidi ya nusu ya kaunti 47 za nchi hiyo ili kuepusha uchaguzi kurudiwa katika duru ya pili.

Uchaguzi wa Keya hadi tunakwenda mitamboni, unaelezwa kuwa ni wa utulivu na kwamba ni kutokana na ukweli kuwa yaliyotokea mwaka 2007 ya watu kupoteza maisha, mali na kukosa makazi hakuna anayeyataka.

Wananchi wamefahamu kuwa haina maana tena kutumiwa na wanasiasa na taifa hilo limejifunza kuwa wanaoumia ni wao wakati wanasiasa wanaendelea na maisha bora.

Kwa mujibu wa mtandao wa televisheni ya Aljazeera, Kenya ina umuhimu wa kipekee kikanda lakini kutokana na mageuzi makubwa ya fikra za uchaguzi yaliyokusudiwa kuzuia ghasia kama zile zilizofanywa baada ya uchaguzi wa 2007, serikali asasi za kiraia na wadau wa amani wamefanikiwa kuwahamasisha wananchi kupiga kura kwa amani.

Kenya ni taifa namba saba kwa uchumi bora barani Afrika na inachukuliwa kuwa moja ya madola yenye demokrasia makini Afrika Mashariki.

Pamoja na hayo ni mzalishaji mkuu wa bidhaa za viwandani zinazouzwa kwenye nchi karibu zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kusini.Na kwa Tanzania ni ndiye mwekezaji mkuu hapa nchini.

Katika maeneo mbalimbali viongozi wameonekana wakionyesha utulivu na upigaji kura uliokomaa, Naibu Rais, William Ruto ametinga wa kwanza kituoni kupiga kura dakika mbili kabla ya kituo kufunguliwa, akisema amewahi kwa vile hapendi kuwasumbua majirani zake, zinasema habari za mtandao wa gazeti la Daily Nation.

Akiongea baada ya kupiga kura saa 12 asubuhi jana katika kituo cha Shule ya Msingi ya Kosachei jimbo la Turbo, Dk. Ruto anasema kwa sababu ya heshima yake na msimamo wa kisiasa anahisi kupiga kura mchana kungesumbua wale ambao wangekuwa wamejipanga kwenye mistari.

"Kila mtu hapa anataka mchakato wa amani. Maombi yetu kabla ya kupiga kura ni kuwa na uchaguzi wa amani. Pia nina furaha kuwa uchaguzi huu wa kihistoria utaleta enzi mpya kwa taifa. Nataka kuhimiza mchakato wa amani," anasema Ruto, ananukuliwa na Mtandao wa Daily Nation.

**MASHINE ZAMGOMEA**

Mtandao wa Daily Nation, unaripoti kuwa mgombea mwenza wa urais wa Ruto wa chama cha Muungano wa Kenya Kwanza Rigathi Gachagua (inasomwa Rigadhi Gashagwa) amezichanganya mashine za bayometriki zinazosoma majina ya wapigakura, ambazo hazikumtambua.

Alama za vidole vyake ziligoma, hazikumsoma ikabidi atambuliwe 'kianalojia' na hatimaye akapiga kura saa 1.39 asubuhi.

Mgombea huyo alipiga kura yake katika kituo cha Shule ya Msingi ya Sagana, jimbo la Mathira, Kaunti ya Nyeri.

Licha ya kwamba kura zimeshapigwa wachambuzi wanauona uchaguzi huwa kuwa wa kielelezo cha ukomavu, kupenda amani na utulivu.

Hata hivyo, wanawaona mashabiki wa Raila kuwa huenda wana jaziba na wangetaka mgombea wao ashinde.

Hata hivyo Raila, hatataka kuonekana kuwa chama chake kinahamasisha machafuko na uhasama nchini Kenya hivyo naye hatakuwa tayari kuwahamasisha vurumai za bada ya uchaguzi, wanasema wachambuzi wa Tanzania.

Raila ana watu wengi wanaomuunga mkono nyumbani Kisumu , wapo Waluya, Wakurya, ukanda wa pwani kama Mombasa, Mijikenda, baadhi ya Wakamba na pia kwa baadhi ya Wakikuyu kutokana na uwepo wa Martha Karua mgombea mwenza.

Ni maoni ya baadhi ya wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaofuatilia uchaguzi huo. Wanatabiri kuwa hali itakuwa shwari kwasababu hamasa za vurugu hazipo na kutoa mfano kuwa mashabiki wa Naibu Rais Ruto, siyo rahisi kuwashawishi na kupata uungwaji mkono wa kufanya vurugu.

"Tunawatazama Wakalenjini , Wakipsigsi, Waborana, Wamasai


INAENDELEA UK.12



Ikulu ya Nairobi . **PICHA: MTANDAO**

# Ndiyo wajihi wa vigogo wanaotamani taji ili kuingia Ikulu ya Nairobi 2022

**Na Mwandishi Wetu**



**RAILA AMOLO ODINGA**

NI mzee kiumri ana miaka 77, amezaliwa katika mji wa Maseno wilayani Kisumu ndani ya jimbo la Nyanza Januari 7 mwaka 1945 . Ni mtoto wa shujaa wa uhuru wa Kenya Jaramogi Oginga Odinga.

Baba yake alikuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Kenya, chini ya awamu ya Rais Jomo Kenyatta.

KAULI MBIU YA UCHAGUZI: Anataka kuwa na Kenya moja, umoja wa kitaifa, maridhiano na ustawi wa Wakenya.

UONGOZI: Anagombea urais kwa mara ya tano, nne zote akishindwa, bila kukubali matokeo.

Mwaka 2018 aliwahi kujiapisha kuwa rais wa Kenya.

Akiwa kiongozi wa Muungano wa Upinzani Kenya (NASA) Raila alijiapisha kuwa rais wa Jamhuri ya Watu wa Kenya mbele ya wafuasi wake jijini Nairobi.

Kuanzia mwaka 2007 hadi 2013 aliandika historia ya kuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Kenya, wakati wa awamu ya Rais Mwai Kibaki (sasa marehemu) .

Amewahi kufungwa jela kwa mashtaka ya kujihusisha na harakati za kutaka Kenya iwe na mfumo wa vyama vingi vya siasa.

TUHUMA: Mwaka 2015 alitajwa kuhusika na tuhuma za ufisadi za kukwepa kodi kwenye



**WILLIAM ARAP RUTO**

Ni mwanasiasa kijana mwenye miaka 55. Amezaliwa Desemba 21, 1966 huko Kemagat nchini Kenya.

Ni msomi ana shahada ya pili ya ekolojia ya mimea (Plant Ecology) akihitimu mwaka 2011 kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi. Lakini hakupoa akijiunga tena na Chuo Kikuu cha Nairobi kwa PhD kwenye sayansi hiyo ya ikolojia na kupata shahada ya juu Desemba 2018.

CHAMA: Anagombea kupitia Chama cha United Democratic Party- UDA chini ya Muungano wa Kenya Kwanza Alliance.

KAULI MBIU: Anachotumia kwenye kampeni za uchaguzi ni kauli mbiu ya kuwajaza Wakenya mapesa, akiwalenga watu wa chini na kuboresha uchumi wao.

UONGOZI: Ni Naibu Rais wa Kenya kazi aliyoanza mwaka 2013 hadi leo.

MSHITAKIWA ICC: Ameacha historia ya kushtakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya ICC. Mwaka 2016 aliburuzwa katika mahakama hiyo iliyoko Uholanzi akishitakiwa kwa makosa ya ukiukaji wa haki za binadamu na ukatili dhidi ya binadamu.

Anadaiwa kufanya makosa hayo baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007, uliompa ushindi mgombea Mwai Kibaki.

UFISADI: Haujamuacha anadaiwa kumiliki mashamba makubwa zaidi ya hekari 40 huko Eldoret, akidaiwa aliyapata 'kiaina.'

***MITANDAO***

# Hakuna matata Wakenya, wanapomaliza jambo lao

**INAENDELEA UK.12**

na Waturkana inavyoelekea ni makundi ya makabila mbalimbali ya jadi siyo kabila moja kubwa ambalo linaweza kuchochewa na kufanya fujo."

"Hawapo kwenye eneo moja kubwa kwa mfano kwenye makazi ya watu wa kipato duni ya Mathare, Kawangware, Kibera na Embakasi , siyo rahisi kuwakusanya, kuwaleta pamoja na kuwachochea kufanya fujo, hivyo amani ni lazima itapewa kipaumbele" anasema mtaalamu wa siasa jina linahifadhiwa.

**KIRANJA MKUU**

Wanasema Kenya inachukuliwa kuwa ni kiranja wa kiuchumi Afrika Mashariki na wawekezaji wengi ambao ni Waasia wakati wa uchaguzi wanaweza kupunguza kasi ya uzalishaji ili kusubiri matokeo, lakini zaidi kuepusha hasara endapo kutakuwa na machafuko.

Yote hayo yanaweza kuathiri biashara Afrika Mashariki kwa sababu Kenya ni mwekezaji mkubwa na mzalishaji wa bidhaa zinazouzwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni 'big brother' huenda wafanyabiashara wa Kenya wasingependa kuangusha uchumi wa Kenya na kusababisha kuparaganyika kwa uchumi wa Afrika Mashariki pia, anaongeza.

"Kuna uwezekano wameliona hilo na wamekubaliana kuwa hakuna sababu za uchaguzi wa fujo wala vurumai, wakirejea pia mkwamo wa kijamii na kiuchumi uliotokana na maradhi ya COVID-19, " anaungwa mkono na msomi mwingine wa Idara ya Uhusiano wa Kimataifa.

**ALAMA ZILIZOACHWA**

Wakati Wakenya wakisubiri matokeo ya uchaguzi huo, wanasema kuwa siasa za Kenya hazina adui wala rafiki wa kudumu, bali kila mmoja anaangalia maslahi yake.

Kwa mfano wanataja mwaka 2007 Mwai Kibaki, alishinda uchaguzi mkuu akawa Rais wa Kenya, wakati huo Ruto alikuwa swahiba wa Mwai na alikuwa Waziri wa Kilimo. Lakini pia ,Ruto alikuwa rafiki kipenzi wa Raila Odinga katika harakati za kuanzisha Muungano wa ODM akishirikiana na Kalonzo Musyoka, Henry Kosgey na William Ruto. Hata hivyo uchaguzi wa mwaka 2022, Ruto anasimama pekee yake na Raila kivyake hawaivi, ikimaanisha kuwa hakuna uadui wala urafiki wa kudumu, kikubwa huenda ni maslahi kupatikana.

Aidha, suala la kulinda maslahi linaonekana pia kwa Rais anayemaliza muhula wake, anamuunga mkono anayeona atalinda maslahi yake ambaye ni Raila.

Ruto naye anatamani kulinda maslahi yake kwa kuhakikisha anabaki Ikulu, kusimamia kila anchoona watu wanakihoji hasa mali alizo nazo, zinazohofiwa kuwa zina maswali mengi.

UCHAGUZI KENYA

# Wakenya wamemaliza kazi sasa ni zamu ya shujaa atakayevikwa taji

**Na Sabato Kasika**




Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akiwasili jana kupiga kura katika kituo cha Gatundu, mji alikozaliwa. **PICHA: ALJAZEERA.**

NAIROBI, Kisumu, Mombasa, KIambuu na kwingineko nchini Kenya mtifuano wa kampeni uliowahusisha zaidi Rais Uhuru Kenyatta na Naibu wake aliyemkataa, William Ruto na upande mwingine Raila Odinga, mpinzani anayeungwa mkono na Ikulu, umemalizika na sasa watu wanasubiri matokeo.

Wakenya waliingia kwenye boksi la kura kuwachagua rais wa awamu ya tano, wabunge, maseneta, magavana na wajumbe wa mabaraza ya kaunti wanaoweza kufananishwa na madiwani kwa upande wa Tanzania, kazi iliyofanyika jana.

Rais Kenyatta amemaliza muda wake na kama ilivyozoeleka angemweka Ikulu Naibu Ruto, lakini sivyo ameegemea kwa mgombea wa Muungano wa Azimio la Umoja, Raila Odinga, ambaye ni mpinzani mkubwa wa Ruto anayewania kupitia Muungano wa Kenya Kwanza.

Wagombea wengine wanaosubiri matokeo ni George Wajackoyah wa Chama cha Roots na David Mwaure wa Chama cha Agano, ambao wanaweza kuitwa wasindikizaji.

Lakini moja ya mambo ambayo yamevuta kampeni za wagombea urais nchini humo na hatimaye uchaguzi uliofanyika jana, ni malumbano makali kati ya Kenyatta na Ruto huku kila mmoja akimrushia mwenzake maneno makali ambayo baadhi ya wachambuzi wa siasa nchini wanayachukulia kama ukomavu wa kisiasa .

Abdukarim Atiki ni mchambuzi wa siasa jijini Dar es Salaam, ambaye anasema nchi hiyo imepiga hatua kubwa kwenye demokrasia inayoruhusu watu kujieleza bila woga kama ilivyoshuhudiwa katika kampeni.

Anaona kwamba malumbano katika kampeni yalikuwa mengi na kwamba demokrasia ya Kenya haimkatazi Rais kuonyesha upande na ametofautiana na Naibu akimuunga mkono Odinga kwa sababu ana nia maalum.

"Naibu amekataa kuingia katika jahazi hilo amebaki kwenye Kenya Kwanza, lakini pia uchaguzi huo unaweza kuwa na matokeo yoyote, kumbuka kuwa kila uchaguzi unapofanyika, Odinga anadaiwa amekuwa akiongoza katika kura za maoni na hata kwenye boksi lakini mwishoni, anashindwa, tusubiri safari hii," anasema Atiki.

Aidha, anasema, Odinga amejaribu kuchanga karata zake, amepata kura asilimia 27 kura za Wakikuyu kule Mlima Kenya, na kufafanua kuwa zamani hilo lilikuwa haliwezekani na kwamba nchi imepiga hatua katika kuelekea umoja wa kitaifa.

"Kenya imepiga hatua sasa kuonekana kwamba makabila yanaweza kukubali kushirikiana, hasa yale yenye uhasimu mkubwa kama Wajaluo, Waluya na Wakikuyu, kwa hiyo magharibi ya Kenya ambayo sasa imeungana na inataka kuhakikisha anachokitaka Rais Kenyatta kinafanikiwa," anasema Atiki.

Aidha, mchambuzi huyo anasema, uchaguzi wa Kenya umekuwa ukitawaliwa na ukabila, na kwamba safari hii ukabila huo huenda ukafutika kutokana na muunganiko wa makabila uliosimamiwa na Ikulu.

"Kwa mfano mgombea mwenza wa Raila, Martha Karua ni Mkikuyu, ameungana na Mjaluo, kwa upande Wakalenjin na Wakikuyu ni jambo la kawaida kama ilivyo kwa Wajaluo na Waluya wote hao wameungana hiyo ni hatua nzuri ya kumaliza ukabila ingawa nchi hiyo bado upo." Anasema.

### MAOMBI YA AMANI

Atiki anasema jambo kubwa ni Watanzania kuwaombea majirani Wakenya uchaguzi huo umalizike kwa amani, kwa kuwa ukivurugika, hata Tanzania inaweza kuathirika, kutokana na mwingiliano wa kibiashara uliopo.

"Tuombe amani itawale wamalize kila kitu kwa amani kwani Tanzania ni mzalishaji muhimu wa malighafi za viwanda vya Kenya, na mbia wa biashara kwa mfano 'supermarket' karibu bidhaa nyingi za viwandani zinazouzwa zinazalishwa Kenya," anasema.

> "Jambo la kuzingatia katika uchaguzi huo ni kila mgombea akubali matokeo ili kuendelea kuifanya nchi kuwa ya amani badala ya kuanzisha vurugu na kusababisha nchi kuingia katika machafuko," anasema.

Anasema Tanzania haijafikia kutengeneza bidhaa za kutosheleza, na kwamba uchumi wa Kenya ukiyumba kwa kutokuwapo kwa amani hata Tanzania itaathirika pia.

"Jambo la kuzingatia katika uchaguzi huo ni kila mgombea akubali matokeo ili kuendelea kuifanya nchi kuwa ya amani badala ya kuanzisha vurugu na kusababisha nchi kuingia katika machafuko," anasema.

### HAKUNA UNAFIKI

Mchambuzi wa siasa Gwandumi Mwakatobe, anasema Wakenya ambacho pia ni cha kujifunza wakati uchaguzi huo unapohitimishwa ni kwamba majirani hao hawana unafiki, wako wazi, na kwamba ndiyo maana Rais na Naibu wake wamefikia kuambiana ukweli hadharani bila woga.

"Unaweza kusema wameshambuliana, lakini ukweli ni kwamba walikuwa wanapashana ukweli pasipo unafiki kwani kwao wana uhuru na uwazi pasipo kufichana ukweli,"anasema Mwakatobe.

Mwakatobe anasema hilo ni jambo la muhimu ambalo wanasiasa wa nchi nyingine hasa za Afrika, wanaweza kujifunza kulifanyia kazi, kwa ajili ya kuambiana kweli pale wanapoona jambo haliendi sawa.

"Binafsi hilo ndilo nililoliona kwenye kampeni za wenzetu, kwamba ni wawazi, hawasiti kuambiana ukweli bila woga kwa manufaa ya taifa lao," anasema mchambuzi huyo anayesema kuambiana ukweli kumesaidia kampeni kufanyika kwa utulivu na amani na kwamba kinachosubiriwa ni Wakenya kwenda katika vituo vya kupigia kura ili kupata awamu ya tano.

Kwa mujibu wa taarifa za DW, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo ya Kenya (IEBC), imeandikisha Wakenya milioni 22 wakiwamo wapigakura 10, 443 wanaoishi ughaibuni, ambao wote wanatarajia kushiriki katika uchaguzi huo.

## MATOKEO UCHAGUZI KENYA

# Ni zamu ya kumsubiri anayepindua meza kibabe, kambi ya Ruto, Raila



Naibu Rais wa Kenya na mgombea urais William Ruto akipiga kura yake jana alfajiri katika kituo cha Shule ya Msingi Kosachei . **PICHA: REUTERS.**

**Na Ani Jozeni**

UPO usemi kuwa 'aliyeumwa na nyoka huchelea akiona kamba usiku'. Kwa Wakenya wanajua athari mbaya za vurugu za uchaguzi, hivyo wako makini, wanapoona kamba hiyo. Kuna jambo kama hilo katika kutabiri nani atakuwa mshindi wa uchaguzi mkuu Kenya, uliofanyika jana.

Pengine kilichowasumbua zaidi wanaoangalia utabiri ni kukosea kubuni au kutabiri kwa usahihi mshindi katika uchaguzi mkuu uliopita, ambako mgombea, Raila Odinga alipewa nafasi kubwa ya kushinda, ila ni Uhuru Kenyatta aliyepata ushindi.

Baadaye wakaungana, maji yalipomfika Uhuru shingoni akakiri kuwa kwa hali iliyokuwepo Kenya isingetawalika, kama 2007.

Kwa maana hiyo, matokeo ya kura ya maoni siyo lazima yalete majibu sahihi, ila siyo hesabu za kupuuzia kwani utafiti unaofanywa kwa makini, na hadi mwisho wa kampeni , kila kura ya maoni iliyotangaza matokeo siyo ya kuongea na watu barabarani ila kwa simu, kwa walioandikishwa kupiga kura, uelekeo dhahiri ni ule wa 'Baba Raila' kushinda.

Kura moja ilitoa pengo la pointi saba kwa Naibu Rais William Ruto kumfikia Odinga, ila maeneo mengi zaidi ya kura za maoni yalionyesha tofauti ya pointi sita.

Kura moja katika mtiririko wa kuonyesha matokeo hayo na mapitio kadhaa ya matazamio hayo ilisema kuwa tofauti hii ya pointi saba au sita inayojirudia kila mahali ni kama uhakikisho kuwa dhamira ya wapiga kura haiwezi kubadilika kwa nguvu au kwa kasi katika siku za mwisho za kampeni, kuleta tofauti katika matokeo ya kura halisi zilizopigwa jana.

Halafu isitoshe hapakuwa na upinzani wa kitaaluma kuhusu kura hizo za maoni, ila kuna sauti moja ilisikika zaidi 'kutuliza munkari'kwa hilo.

Sauti hiyo ni ya Moses Kuria, mbunge wa Gatundu Kusini aliyeonekana kufadhaishwa na matokeo ya kura ya maoni ya TIFA (Trends and Insights Africa) mnamo Julai 13, ambayo ilionyesha kuwa Raila anaongoza. Ubishi wa mbunge huyo ulikuwa wa kisiasa kwa upande mmoja na wenye ladha ya kitaaluma (ukusanyaji habari) kwa upande wa pili, akisema 'unafanya kura zake za maoni nchini kote.'

Kwa vile ni mbunge, baadhi ya wataalamu na wasikilizaji wake walingonja au kufuatilia anatoa 'vipande' gani kuhoji kile TIFA walicholeta, ambacho kimsingi hakikuhojiwa na watalamu wengine wa kura za maoni.

Jambo la kushangaza ni kuwa Kuria aliwahi kutangaza matokeo ya kura za maoni ambazo alihusika nazo akiwa kama kiongozi wa Chama Cha Kazi (CCK) Oktoba 2021 ambako katika kupiga kura kati ya wagombea wawili, Raila na Ruto, ni Raila angeibuka mshindi, lakini kura zikitawanywa kwa wagombea wanne wamaofahamika zaidi (waliobaki ni Musalia Mudavadi ambaye yuko na Ruto sasa) na pia Kalonzo Musyoka (ambaye siku za mwisho wa kutangaza majina ya wagombea, alijiunga na kambi ya 'Baba'). Hivyo Ruto angekuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuongoza. Kilichopo sasa ni wale wawili, si wanne tena.

Pamoja na hisia hizo au vielelezo hivyo vya kitaaluma, au vyenye sura ya kitaaluma kwani alitoa hata asilimia alizotarajia, baadaye ikaonekana mwelekeo wake wa kisiasa kuwa bora zaidi kuliko jitihada zake za kitaaluma. Mtawanyo wa kuungwa mkono katika kura hiyo ya maoni Oktoba mwaka jana iliwaonyesha 'watia nia' wakuu wanne wakiwa kama vile wanakabana koo, ila sivyo ilivyotokea baadaye. Kutokana na muafaka wa Raila na Uhuru, kambi hiyo imekuwa kubwa mno hivyo kufanya Ruto awe 'mtia nia' pekee ambaye ana uwezo, angalau kwa mbali, kuisumbua kambi hiyo.

Wengine ilibidi watafute maskani, na siyo kama wagombea wenza kama walivyotaka, ila kama washiriki.

Hata hivyo mbunge na mwanahabari mtafiti Kuria ameendelea kutikisa anga za kura za maoni akijaribu iwezekanavyo kumweka mbele Ruto, ambaye anapendwa na wanasiasa wengi wa Ukanda wa Kati nchini humo wasiopenda maridhiano ya kitaifa ambayo kwa miaka minne sasa yanasimamiwa kwa pamoja kati ya Rais Kenyatta na kiongozi wa ODM (Orange Democratic Movement), Raila Odinga.

> Kuna wakati alijaribu kuunda umoja mpya nchini humo na hasa kuunganisha wanasiasa ukanda wa kati, akiwa na Martha Karua mgombea mwenza wa Raila na Mwangi Kiunjuri, ila jitihada za aina hiyo zinakwama katika kupata kiongozi.

Wanataka mtindo wa'vyama' na siyo kujenga madaraja kati ya pande tofauti za nchi na ngome yao ni Ukanda wa Kati na Bonde la Ufa. Yako maeneo mengine siasa za kubahatisha zinawasaidia, hususan kwa walalahoi.

Kiongozi huyo wa 'Chama Cha Kazi' ambaye hakuwa na ubavu wa kugombea nafasi hiyo ya juu amejipatia umaarufu kama mpiga debe mahiri wa Ruto, ila miezi ya karibuni alifanya juhudi za kujitenga kidogo na kampeni ya Naibu Rais, ili aongee kwa ufasaha zaidi kama mchambuzi wa mwelekeo wa uchaguzi mkuu.

Kuna wakati alijaribu kuunda umoja mpya nchini humo na hasa kuunganisha wanasiasa ukanda wa kati, akiwa na Martha Karua mgombea mwenza wa Raila na Mwangi Kiunjuri, ila jitihada za aina hiyo zinakwama katika kupata kiongozi.

Isitoshe, ingebidi kwanza wachague kati ya kambi hizo mbili kuu umoja huo uko upande gani na kwa hilo walitawanyika.

Kuanzia wakati Raila alipotangaza nia ya kugombea, au kuchukua fomu ulipowadia kwani yeye na Uhuru walikuwa wakijitahidi kuweka pembeni masuala ya uchaguzi mkuu na badala yake kuendelea na sera za kujenga madaraja na hata kubadili katiba kuweka mazingira tofauti kwa taswira ya jitihada hiyo.

Hatua hizo miezi iliyopita zilikwama baada ya Mahakama Kuu ya Rufani, kubatilisha sheria iliyopitishwa kwa lengo hilo pale kambi ya Ruto ilipeleka shauri hilo kwa dhima hiyo hiyo kuwa linavunja katiba ya Kenya ikashinda, iwe ni sheria au harakati.

Labda kuna somo moja la ushindani huo pamoja na kura za maoni, kwamba siyo jambo la ajabu kwa nchi kuendesha uchaguzi halisi wa kidemokrasia ambao tangu awali hutoa uwezo kwa sauti zote kujieleza na kukubaliwa kwake miongoni mwa wananchi kuweza pia kupimwa katika kura za maoni.

Tatizo ni kukosekana mabadiliko ya kina ya uchumi watu binafsi kustahimili kubadilika uongozi wa nchi bila kutetereka, au kuanza kwa njama za kubadili matokeo kama Kenya awali. Pale sekta binafsi inachechemea nyuma ya uchumi dola wa taasisi za serikali, haitakuwa rahisi kufanya uchaguzi kidemokrasia.





## TANAPA yahamasisha wananchi utalii wa ndani

**Magdalena Jackson na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limetoa wito kwa Watanzania kufanya utalii wa ndani na kuangalia fursa za uwekezaji zilizoko kwenye hifadhi hizo.

Aidha, imetangaza ofa kabambe kwa Watanzania kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja vya maonyesho ya Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma, Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Fredrick Malisa, alisema lengo ni kutangaza vivutio na kuendeleza kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan ya filamu ya The Royal Tour na kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko katika hifadhi.

"Kwa mfano Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kuna maeneo 22 ya uwekezaji. Kuna sehemu za kujenga kambi za muda na za kudumu na kujenga hoteli, hivyo TANAPA inatoa fursa kwa wananchi kuwekeza katika maeneo hayo," alisema.

Pia alisema kuna baadhi ya Watanzania bado hawana elimu kuhusu umuhimu wa hifadhi mbalimbali zilizoko nchini, hivyo shirika hilo limedhamiria kutoa elimu kuanzia shuleni ili watoto wadogo wapate uelewa chanya wa hifadhi hizo.

"Hii ofa kabambe ya Tarangire ni Sh. 93,000 kwa mtu mmoja kwa safari ya kwenda na kurudi pia kwa Sh. 117,500 kwa safari ya kulala," alisema.

Katika hatua nyingine, Ofisa wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Sharif Mohammed Mzee, alishauri wajasiriamali kutumia fursa ya maonyesho hayo kuonyesha bidhaa zao mbalimbali na kujifunza mbinu za kuboresha biashara zao.

Alisema maonyesho hayo yanapofanyika, yatumike katika kuboresha na kubuni bidhaa zenye ubora ili kuingia kwenye ushindani wa masoko ya ndani na nje.

Pia alisema bado kuna umuhimu wa watu kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa kwenye maonesho ya wakulima na ziwabadilishe kiuchumi kupitia elimu zinazotolewa kupitia kwa wafugaji, kilimo, afya, elimu na kwenye taasisi za kifedha.

**"Hii ofa kabambe ya Tarangire ni Sh. 93,000 kwa mtu mmoja kwa safari ya kwenda na kurudi pia kwa Sh. 117,500 kwa safari ya kulala," alisema.**

# Tume yakiri udhibiti mbovu ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imebaini bado kuna mifumo mibovu ya udhibiti wa ndani katika vyama vya ushirika, hivyo kusababisha upotevu wa fedha na mali za ushirika.

Ukaguzi uliofanywa katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022 kwenye vyama 6,013 kati ya 9,185, ulibaini tatizo hilo huku mashauri 23 yakifunguliwa kwenye mahakama mbalimbali nchini.

Akitaja mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2021/22 na mwelekeo wa mwaka 2022/23 jana jijini hapa, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema pia ukaguzi huo ulibaini kuwapo kwa ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji wa vyama hivyo.

Aidha, alisema baadhi ya vyama vinashindwa kuandika miamala ya fedha kulingana na taratibu za fedha zilizoko.

"Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwaondoa au kuwatengua viongozi 17 wa bodi za vyama viwili vya upili na wajumbe 224 wa bodi katika vyama vya msingi 32 kutoka mikoa 15 walioshindwa kusimamia vyama vyao ipasavyo," alisema.

Kadhalika, alisema viongozi waliobainika kuhusika na vitendo vya wizi na ubadhirifu wamefikishwa kwenye vyombo vya dola kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria.

"Kesi 23 (madai 21 na jinai 2) zimefunguliwa kuhusu mashauri mbalimbali ya vyama vya ushirika katika mahakama kote nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema viongozi 17,423 na wanachama 197,968 wa vyama hivyo walipatiwa mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vyama.

Kuhusu mwelekeo wa mwaka 2022/23, mrajis huyo alisema tume imejipanga kufanya mambo tisa ikiwamo kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuchochea maendeleo ya ushirika nchini.

"Kufanya uthamini wa mali zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutambua thamani halisi ya soko ya mali hizo na hivyo kuviwezesha vyama kufanya uwekezaji wenye tija," alisema.

Dk. Ndiege alisema wamejipanga kuanzisha Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za SACCOS utakaotumika kama kinga ya akiba na amana za wanachama pindi SACCOS zao zitaposhindwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

"Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika kwa kutoa mafunzo kwa maofisa ushirika 226, kukagua vyama vyote na kuendelea kununua vitendea kazi na kununua magari kwa ajili ya kuongeza tija kwa maofisa ushirika," alisema.

Alisema watatengeneza utaratibu wa uwezeshwaji vyama vya ushirika ili kuongeza ufanisi.




Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika la Nyumba za Taifa (NHC), Muungano Saguya, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji na mwelekeo wa shirika hilo kwa bajeti ya mwaka 2022/2023 ambapo wanatarajia kuanza mradi wa nyumba 5,000 ujulikanao kwa jina la Samia Housing Scheme na utagharimu Sh. bilioni 466 . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC ataka wafugaji, wakulima na wavuvi kushiriki katika sensa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wakulima, wafugaji na wavuvi kushiriki sensa ya watu na makazi na kutoa takwimu sahihi zitazosaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo ya sekta hizo.

Senyamule alisema hayo juzi jijini hapo alipokuwa akifunga maonyesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Kati.

"Kila mmoja wenu ahakikishe kuwa sensa haimpiti ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi zitakazotumika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo ya sekta hizi.

"Lakini mnapaswa kutoa takwimu sahihi katika sensa ya mwaka huu. Yako maswali mengi katika dodoso, hivyo kila mmoja atoe takwimu sahihi kwa makarani ili kujua idadi ya mifugo na kuwezesha kupatikana kwa huduma mbalimbali kama vile majosho kwa ajili ya mifugo yenu," alisema Senyamule.

Pia aliwataka wafugaji kushiriki uvishaji wa hereni mifugo kazi ambayo inaendelea nchini ili kuiwezesha serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupata idadi sahihi.

Vilevile, aliwataka wakulima na wafugaji kutumia maonyesho hayo kubadili utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zao.

"Tunapaswa kubadilika katika ufugaji ili kufuga kibiashara na kulima kibiashara. Hivi sasa hatupaswi kuangalia idadi ya mifugo au ukubwa wa shamba bali kinachopaswa kutazamwa ni uzalishaji wa mazao. Tumeona leo (juzi) kuna ng'ombe ambaye anatoa maziwa lita 36," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa pia aliagiza halmashauri zote za mkoa wa Dodoma kwenye maonyesho ya mwaka ujao, kuandaa utaratibu wa kupeleka wakulima ili kujifunza kilimo bora na chenye tija.

"Lakini eneo hili wakati ambapo maonyesho yanaisha panabaki bila kitu cha kufanya, hivyo naagiza kuangalia utaratibu ambao utawezesha kujengwa kwa hosteli ambazo zitatumiwa na wakulima kutoka katika halmashauri zetu na kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo za kisasa kwa awamu," alisema. Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Muhina, aliwataka wakulima kujiwekea utaratibu wa kuhifadhi malisho ya mifugo yao.

"Mwaka huu tumepoteza mifugo mingi sana kwa iliyokufa kutokana na kukosa malisho, hivyo wafugaji mnapaswa kuhifadhi malisho ili kuondoka na hali hii lakini tunapaswa kutunza vyanzo vya maji ili kuwa na ufugaji endelevu na wenye tija," alisema.



# Rais Samia aridhishwa na TARI utafiti wa mafuta

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema anaridhishwa na kazi kubwa inayofanywa na watafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) katika mkakati wa kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Rais Samia alisema hayo baada ya kupata maelezo ya taasisi hiyo kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, baada kutembelea banda la wizara hiyo pamoja na taasisi zake katika kilele cha maonesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, mkoani hapa.

Waziri Bashe, alimweleza Rais Samia kupitia taasisi za TARI, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), zitazalisha mbegu bora za alizeti tani 5,000 ambazo zitasambazwa kwa wakulima.

Alisema hatua hiyo itawawezesha wakulima kuzalisha alizeti nyingi ambayo itakamuliwa na kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula nchini na kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta.

Waziri Bashe alimshukuru Rais Samia kwa kuongeza bajeti ya utafiti kutoka Sh. bilioni 11 hadi kufikia Sh. bilioni 40 kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Alisema fedha hizo zitatumika kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kwa mazao mbalimbali nchini ikiwamo yanayozalisha mafuta ambayo ni alizeti na michikichi.

Waziri Bashe, alisema wizara imejenga uwezo wa taasisi hiyo kupitia Kituo cha Mlingano, kilichoko mkoani Tanga kufanikisha ukusanyaji wa sampuli za udongo nchi nzima, kuzipima katika maabara na kutoa majibu ya afya ya udongo ikiwa mojawapo ya kuwasaidia wakulima kufanya uwekezaji wa kilimo bora.

"Kupitia kituo cha Mlingano, tunapima udongo wa shamba lolote la mkulima na tunampa majibu ya muda mfupi kama anahitaji kuongeza mbolea anashauriwa ili kufanya kilimo chenye tija," alisema Waziri Bashe.

Alifafanua kwa kutumia kituo hicho cha Mlingano, wakulima wanashauriwa matumizi ya mbolea kwa mazao wanayoamua kulima katika mashamba yao ili kuzalisha kwa tija na kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo.

Kuhusu upatikanaji wa mbegu bora za mahindi, Waziri Bashe alimweleza Rais Samia kuwa wizara yake inaweka nguvu kuhakikisha mbegu hizo ambazo ni chotara UH6303, inayofaa kwa ukanda wa Nyanda za Juu Kusini zitazalishwa kwa wingi ili iweze kusambazwa katika ukanda huo.

Alisema hivi sasa jitihada zinaendelea kuhakikisha mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na TARI zinazalishwa na ASA ili ziweze kupatikana kwa wakulima kwa bei ndogo ya serikali.

Waziri Bashe alisema, ili kuwa na vyanzo vya vinasaba vya utafiti wakati wote, wizara hiyo imeanza kukusanya na kuhifadhi mbegu za asili zisipotee kwa matumizi ya sasa na ya baadaye.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, aliahidi kufanyia kazi maelekezo ya Rais Samia kuhakikisha mbegu bora za kutosha zinapatikana ikiwamo zinazozalisha mafuta.



Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga (kushoto), akiangalia mbegu mbalimbali za mazao ya mikunde, zilizofanyiwa utafiti na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ilonga, mkoani Morogoro, alipotembelea maonyesho ya kilimo Nanenane, jijini Mbeya juzi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Utumishi yatoa elimu uombaji ajira mfumo mtandao

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

OFISI ya Sekretarieti ya Ajira na Utumishi wa Umma imeyatumia maonesho ya wakulima Nanenane kutoa elimu kwa wananchi ya namna ya kutumia mfumo wa Ajira Portal kuomba ajira.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la ofisi hiyo kwenye maonesho hayo, Geofrey Kikosa kutoka Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira na Utumishi wa Umma alisema, wamekutana na wateja/wadau mbalimbali waliofika kwenye banda lao na kuwaelimisha kufanya mchakato huo.

"Katika maonesho haya ya Nanenane tumekutana na wadau kusikiliza changamoto wanazokabiliana nazo hasa wakati wa uombaji wa ajira hadi wakati wa usaili, na baada ya kuwasikiliza pia tumewasaidia kutafuta suluhu ya changamoto zao pamoja na kupata maoni ya wadau kuhusu mchakato wa ajira unavyoendeshwa," alisema Kikosa.

"Wadau wengi waliojitokeza kwenye banda letu wameonyesha kuhitaji msaada katika eneo la usajili na sisi tumewaelekeza ukubwa wa picha unaotakiwa uwekwe na kuwaelekeza namna ya kufanya usajili vizuri katika akaunti zao ikiwamo kuhakiki vyeti vyao kwa mawakili au wanasheria," alisema Kikosa.

Vile vile, alisema wamepata maoni katika eneo la kushindwa kuomba nafasi mbalimbali zinazotangazwa katika taasisi mbalimbali na wameitumia changamoto hiyo kama fursa ya kutoa elimu zaidi katika eneo hilo.

"Wadau wengi wamekuwa na sifa za juu na tumekuwa tukiwaelekeza waombe nafasi kwa mujibu wa kiwango cha elimu ya nafasi inayotangazwa, pia tumepata changamoto ya wadau kusahau neno la siri na tumewaelekeza namna ku-'reset' (kurudisha) hilo neno siri ili kupata neno siri jipya," alisisitiza Kikosa.

Hata hivyo, aliwaasa wadau na waombaji ajira katika utumishi wa umma kufika katika ofisi zao au kutembelea tovuti yao ili kuona maelekezo ikiwamo kupata namba za simu kwa ajili ya kupiga na kupata huduma wanazozihitaji.

Naye Adeline Seka, alisema elimu waliyoipata kuhusu ajira portal itawasaidia kwa kiasi kikubwa uombaji ajira matangazo yanapotolewa.

Alifafanua kuwa walikuwa wakipata shida kwenye uombaji, lakini baada ya kuelimishwa wanaamini haitaleta shida wakati mwingine serikali inapotangaza ajira.

## Wakulima pareto wapewa fursa kuongeza uzalishaji

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

SERIKALI imewataka wakulima wa zao la pareto nchini kuongeza uzalishaji kutoka tani 2,000 hadi kufikia 5,000 ili waweze kukidhi mahitaji ya viwanda vinavyonunua zao hilo nchini.

Hayo yalisemwa na Mdhibiti wa zao la Pareto wa Bodi ya Pareto nchini, Edwin Margwe katika maonyesho ya Nananane kitaifa yanayoendelea kwenye viwanja vya John Mwakangale.

Alisema uhitaji wa zao hilo hivi sasa ni mkubwa na wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo ili kupanua wigo wa soko nchini na nje ya nchi kwa kulima zao hilo kwa wingi.

Alifafanua zaidi ya kuwa awali ilikuwa kampuni moja ambayo inanunua zao hilo, lakini hivi sasa kampuni zimeongezeka na uhitaji umeongezeka ndio maana wanahimiza wakulima kulima zao hilo kwa wingi.

"Naomba wakulima wa zao hili muongeze jitihada kuhakikisha mnalima zao hilo kwa wingi ili muweze kujiinua kiuchumi," alisema Margwe.

Alifafanua kuwa wakizalisha kwa wingi watasaidia kutosheleza uhitaji wa zao hilo nchini.

Akizungumzia suala la mbegu, alisema wanashirikiana pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini ili kuhakikisha wanapata mbegu bora kwa ajili ya wakulima kwenda kupanda katika maeneo mbalimbali.

Aidha, aliwataka vijana kujikita katika kilimo hicho kwa kuwa kwa sasa kuna soko kubwa kutokana na mnyororo wa thamani wa matumizi ya zao hilo mashambani na majumbani.

Naye Mratibu wa zao la pareto, Michael Bishubo kutoka kampuni ya PCT, alisema moja ya faida ya viuatilifu ni kwa ajili kusaidia kukabiliana na wadudu waharibifu wa shambani na majumbani.

Akielezea namna ya pareto inavyotumika kama viuatilifu alisema inapopandwa shambani maua na yake ndiyo yanavunwa na kilichomo ndani ya maua ni kiuatilifu maua ambacho kinaenda kuchujwa na kutumika kama dawa ya kwenda kuua wadudu shambani.

Alifafanua kuwa wanyama wanapokula machicha husaidia kuondoa minyoo ambayo husumbua wanyama.

"Naomba vijana wajitokeze kulima zao la pareto kwa sababu lina soko kubwa ndani na nje ya nchi," alisema Bishubo.

Hata hivyo, aliiomba serikali kuendelea kuweka msisitizo katika zao hilo ili wakulima wajitokeze kulima kwa wingi.

Pia, ameziomba taasisi za fedha kutoa elimu kwa utoaji mikopo kwa wakulima ili wengi wao waweze kujitokeza kukopa.



# Utoro wanafunzi bado tatizo sugu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Shirika la Elimu kwa Wote la Qatar (EAC) kuendesha mradi wa kuwarejesha shule wanafunzi watoro, bado tatizo la utoro wa wanafunzi lipo hasa kwa shule zilizoko katika visiwa vidogo ndani ya Zanzibar.

Akizungumza jana na Nipashe, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi katika Kisiwa cha Kojani Mkoa wa Kaskazini Pemba, Khamis Ali Makame, alisema zaidi ya watoto 200 wako nje ya mfumo wa elimu kisiwani humo kwa sababu ya utoro.

Alisema watoto hao wana umri kati ya miaka saba na 14 ambao baadhi yao wametoroka shule na wengine hawajaandikishwa kabisa.

Khamis alisema wizara ya elimu kupitia mradi wa kuwarejesha shuleni watoto unaofadhiliwa na EAC, wanafunzi 63 wamerejeshwa na wanaendelea vizuri na masomo yao shuleni hapo.

Mwalimu huyo alitaja sababu kuu tatu zinazofanya wanafunzi kutoroka shule ni umasikini wa wananchi wa kisiwa hicho, uliosababisha ajira binafsi kwa watoto ikiwamo uvuvi, uhaba wa walimu shuleni na mwamko mdogo wa baadhi ya wazee kuhusu umuhimu wa elimu.

Kuhusu uhaba wa walimu, alisema shule hiyo ina wanafunzi 2,256 wakiwamo wa maandalizi ni 379 wenye walimu wanne wakati msingi ina wanafunzi 1,877 ikiwa na walimu 23 ambao hawatoshelezi kulingana na idadi hiyo.

"Uhaba wa walimu nao unachangia utoro wa wanafunzi shuleni kwa sababu mwanafunzi anapoona mwalimu hajaingia darasani kufundisha, anapata mwanya wa kutoroka shule," alisema.

Pia mwalimu huyo alisema kutokana na jiografia ya Kisiwa cha Kojani, inawalazimu baadhi ya walimu kuvuka bahari kutoka ng'ambo nyingine wanakoishi na kwenda kufundisha Kojani kwa sababu hakuna nyumba za walimu kisiwani hapo.

Alisema kati ya walimu 27 wanaofundisha kisiwani hapo, 11 wanaishi nje ya kisiwa na hulazimika kila siku kuvuka bahari kwa kutumia usafiri wa boti ndogo ambazo zina changamoto zake.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, walimu hulazimika kwa kila siku kutumia Sh. 1,000 kwa ajili ya usafiri na wanadai hela ya nauli kwa muda wa miaka mitatu hawajalipwa na serikali, hivyo hulazimika kutoa fedha zao ili kutimiza majukumu yao ya kazi.

"Mimi binafsi siishi katika kisiwa hiki naishi kijiji cha Mchanga mdogo na hulazimika kuvuka bahari kila kila siku. Huu mwaka wa 30 nafundisha shuleni hapa," alisema.

Hivi karibuni Chama cha Walimu Zanzibar, kilikumbushia madeni wanayodai walimu ikiwamo mrundikano wa deni la nauli na posho.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madeni yao, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Haji Juma Omar, alisema bado walimu wa shule za sekondari wanadai fedha za nauli tangu Agosti, mwaka jana na walimu wa shule za msingi wanadai tangu mwaka 2019.

## SMZ yatoa umuhimu makundi maalum sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka huu imezingatia na kutoa kipaumbele kwa makundi na watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo watu wenye ulemavu.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Salum Kassim Ali, alisema hayo jana mjini hapa alipozungumza na maofisa wa sensa ambao wanashughulikia makundi maalumu ya watu wenye ulemavu.

Alisema sensa inalenga kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanafikiwa kwa ajili ya kuhesabiwa ili kujulikana idadi kamili na aina ya ulemavu wao.

Salum alisema moja ya changamoto kubwa sasa ni kwamba idadi kamili ya watu wenye mahitaji maalumu na wenye ulemavu kwa kuwa hadi sasa haifahamiki kikamilifu.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali inataka kufahamu mahitaji ya watu wenye ulemavu kulingana na aina ya ulemavu wao na njia pekee ya kufahamu hayo ni kuwapo kwa sensa.

Aliwataka watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 hatua ambayo serikali itaiwezesha kufahamu idadi kamili ya watu wake pamoja na mahitaji kwa ujumla wake. Naye Mkufunzi wa Sensa ya Watu na Makazi, Ashura Hassaan Othman, alizitaka jumuiya zote zinazowashirikisha watu wenye ulemavu kuona kwamba wanafikiwa na kuorodheshwa katika sensa ya watu na makazi kwa mafanikio makubwa.

Alisema ni muhimu serikali kufahamu idadi kamili ya watu wenye ulemavu nchini pamoja na aina ya ulemavu wao kwa ajili ya kuwapatia huduma muhimu zitakazosaidia na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.




Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said (kulia), akikabidhi zawadi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Rajab, baada ya kufungua mdahalo wa kijana imara ulioandaliwa na Kiona Youth Coordinates (KYCo), jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi ataka lugha nyepesi utafiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka watafiti kuwa na utamaduni wa kuchapisha matokeo ya utafiti kwa lugha nyepesi na rafiki ili jamii ielewe na kunufaika nao.

Aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, wakati akifungua kongamano la 16 la Jumuiya ya Wanazuoni na Watafiti wa Mambo ya Kale katika ukumbi wa Chuo cha Utalii, Maruhubi Zanzibar.

Aliwataka kutafsiri taarifa za utafiti pamoja na mapendekezo ya uboreshaji wa maeneo ya utafiti huo ili kwa pamoja viwe sehemu ya vivutio vya utalii. Dk. Mwinyi alisema taaluma ya mambo ya kale na urithi wa utamaduni vinagusa sekta zate za kiuchumi, kijamii, kisiasa, teknolojia na mazingira yakiwamo magonjwa mbalimbali, hivyo ni tegemeo kubwa la taifa kufahamu nchi ilikotoka, ilipo na inakokwenda kuwa utafiti unatoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa malengo yanayopangwa nchini.

Alisema anatamani kuona Zanzibar na maeneo mengi ya urithi wa utamaduni kwingineko barani Afrika yakipokea watalii wengi kama ilivyo Gorée Island kule Senegal na Roben Island, Afrika Kusini.

Dk Mwinyi katika hotuba yake hiyo, alisema kuna maeneo mengi ambayo hayajafanyiwa utafiti na yanawasubiri watafiti, hivyo kupitia kongamano hilo, aliwakaribisha kufanya utafiti Zanzibar hususan katika akiolojia ya bahari.

Alisema serikali yake, sera kuu ya kiuchumi ni uchumi wa bluu ambapo utajiri wa urithi ulioko baharini unaweza kutumika kama fursa ya kukuza sekta hiyo Zanzibar kupitia utalii.

"Serikali ninayoingoza inatoa sana kipaumbele kwa sekta yenu ndiyo maana tuliunda wizara kamili inayoshughulikia mambo ya kale. hivyo ni matarajio yangu kwamba mtakuja kufanya utafiti Zanzibar na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Rais aliwahakikishia watafiti wote wanaotaka kufika Zanzibar kuwa milango ya kufanya utafiti iko wazi na mazingira ya ufanyaji wa utafiti ni mazuri na utaratibu wake ni rahisi na nafuu kwa kuwa humchukua mtafiti siku mbili hadi tatu kupata kibali na ruhusa ya kufanya utafiti.

Aidha aliwataka washiriki wa kongamano hilo kutoka nchi mbalimbali duniani kutenga muda wao kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Zanzibar na Tanzania na kwamba hiyo itasaidia kuona hali ya ukarimu na usalama nchini Tanzania.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAMADHANI H. KANJOE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1094-0283** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **JIHAD SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI **TAARIFA: DAR/CHU/RB/313582/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA:01/2022**

**JASON ERNEST KAINDOA ............................MWOMBAJI**
**(Representative or Dr. Projestus Kweyamba )**

**DHIDI YA**

**GLORIA FRANCIS ..............................MJIBU MAOMBI**

**KWA: GLORIA FRANCIS**
**(POPOTE PALE ULIPO )**

Unaarifiwa kuwa maombi Na 01/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 07.09.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2:30 asubuhi

Hivyo, unaamuriwa kuhudhulia wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 01.08.2022

MWENYEKITI
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MBOZI LILILOPO SONGWE**

**SHAURI NA.22/2022**

**TUMWITIKE KASHIRIRIKA..........MDAI**

**DHIDI YA**

**ADAM MTEGA..............................MJIBU MAOMBI WA 1**
**NESMO SHOMBE.........................MJIBU MAOMBI WA 2**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA: ADAM MTEGA**

Fahamu kwamba TUMWITIKE KASHIRIRIKA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 12.08.2022,saa 2:30 asubuhi,mbele ya Mh.T.Munzerere ,mwenyekiti wa baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba,Songwe.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Vwawa,Mbozi mjini.
Kumbuka:Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahiki ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 29/07/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA
SONGWE
TANZANIA

T.MUNZERERE
MWENYEKITI
29/07/2022

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 595/2021.**

**THE REGISTERED STRUSTEDES OF MUTAMAR TAALIM ALIS ISLAMIC —- MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ELIAS KOMBA —-WAJIBU MAOMBI**

**WITO KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi Namba tatu unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 29/08/2022 saa 2:00 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwaajili ya kuleta hati zenu za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili usikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

**Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo 04/07/2022**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANK GEORGE KWAVAVA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRIES** yenye **USAJILI NAMBA T 325 DGG** . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/313656/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 681 OF 2022**
**IN THE MATTAER OF THE ESTATE OF THE LATE JACKSON GRIFFIN MWAIPOPO and**
**In the application for letters of administration**
**by**
**GODWIN GRIFFIN MWAIPOPO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above –named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 6 day of September 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 27 day of JULY 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**MASOLWA JUMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0713-0036** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IGUNGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2004 na cheti cha ualimu chenye namba ya usajili **E0518-0259** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU NDALA mwaka 2008. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **IGU/RB/908/2022**

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

**FRANCIS JOSEPH ITENGEJA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili, **T 754 AKP**
Chasis Namba: **5X805072371**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/299962/2022.**

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**NASORO Y MAGINGA ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **PIKPIKI(HAOJE)** yenye namba za usajili **MC 440 AJK**
Chasis Namba: **LC6PCJK26E0003417**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/314441/2022.**

---

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**SEMENI JIRANI SALUM** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba za usajili **TAE256614** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi-UHAMIAJI Dar Es Salaam mwaka 2019,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha poliasi. Polisi taarifa **DAR/STA/RB/312424/2022**

---

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**BENO JOHN MGATA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya PIKPIKI yenye namba za usajili **MC 423 CEN**
Chasis Namba: **MD2A211BY3KWL89170**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/300030/2022.**

---

**RE: THE LAND ACT NO.4 OF 1999**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF;**
**REF: NO.CDA /ED/LA-15/37045**
**REGISTERED OWNER: VERONICA JULIUS MSANJILA**
**LAND: PLOT NO. 41 BLOCK 'F' ILAZO WEST**
**APPLICANT: VERONICA MSANJILA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land describe above is said to be lost and that intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LATER OF OFFER** in lieu there of unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** if found, should be delivered at the Office of the;
Director General,

**CAPITAL DEVELOPMENT AUTHORITY,**
**P.O.BOX 913, DODOMA.**

Issued by
**DIRECTOR GENERAL**
**CAPITAL DEVELOPMENT AUTHORITY**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NUHU DAVID NYAMBULAPI,** Anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Toyota Premio yenye no za usajili **T 242 ARD,** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/CHU/RB/843488/2020**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GLOBAL LEADER ENTERPRISES LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA BREVIS** yenye usajili namba **T 713 DCQ .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MBE/MBA/RB/195438/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHRISOSTOM DANIEL MASAGIDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 635 APK** aina ya SAN-LG. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NY/RB/275657/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MBARAKA MOHAMED AHMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISSAN MURANO** yenye namba za usajili **T.734 CAM.**
Yenye Engine namba **QR25302090A** na Chassis namba **TZ50007525.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa **Polisi:TAN/RB/314632/2022**

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

Ndugu **FORTUNATUS KABYEMERA KAJUNA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Corona Premio ambayo imesajiliwa kwa jina la **GODSON KACHEOKOLELA WILLISON** lenye namba za usajili **T993 DLL,** injini namba **7AJ203934** na Chassis namba **AT2110140136.**
Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/313739/2022.**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0624268347.**

---

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**THE GIFT ARENA LIMITED NAMBA YA KAMPUNI: 124951**
**TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI KIKAO CHA MWISHO.**
Bodi ya wanahisa wa **THE GIFT ARENA LIMITED** imeamua kufunga shughuli zake za biashara rasmi na kikao cha mwisho kinatarajia kufanyika **tarehe 11/08/2022** ofisini **plot No 499/101** mtaa wa Jamaat, Ilala Dar es salaam.
Kwa yeyote mwenye pingamizi awasiliane na mfilisi wa kampuni kwa kupitia mawasiliano: **JINA: LINDA E. LUGANO NAMBA YA SIMU: 0716393252**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yaendeleza mashambulizi Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

UINGEREZA imesema katika siku za mwishoni mwa wiki Russia iliendelea kujiimarisha kiulinzi kusini mwa Ukraine, huku ikielekea mji mkuu wa Kyiv kutokea mkoa wa Donetsk kwa upande wa mashariki.

Katika taarifa yake, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema kwa takribani siku 30 zilizopita mji wa Bakhmut umekuwa lango la kuingilia majeshi ya Russia kwa upande wa mashariki ya Donbas, na wamefanikiwa kusonga mbele kwa umbali wa kilometa 10 katika eneo hilo.

Taarifa hiyo iliongeza kusema katika maeneo mengine ya kimkakati, Urusi imekuwa ikifanya majaribio ya kupunguza nguvu za kijeshi za Ukraine, lakini katika kipindi hicho cha siku 30 zilizopita imeshindwa kusonga mbele kwa umbali wa hata kilomita 3, ikiwa ni pungufu ya vile ilivyopangwa. **DW**

# Ujerumani kujadili sheria kuzuia maambukizo

**BERLIN,** UJERUMANI

MAWAZIRI wa Afya wa majimbo ya Ujerumani wanakutana leo (jana )katika mji wa Magdenburg kujadili rasimu ya sheria ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, lengo la suala hilo ni kuzifanyia marekebisho kanuni zake, katika kukabiliana na janga la virusi vya UVIKO-19.

Pia ilibainishwa kuwa wiki iliyopita Waziri wa Afya wa Ujerumani, Karl Lauterbach na mwenziwe wa Sheria, Marco Buschmann, waliwasilisha hatua mpya za kukabiliana na virusi vya Corona ili ziweze kutumiwa katika msimu ujao wa mapumziko.

Iliripotiwa kuwa pamoja na mambo mengine katika rasimu hiyo inataka uvaaji wa barakoa kuwa wa lazima katika safari za muda mrefu za treni na ndege, vilevile kuvaliwa katika hospitali na vituo vya afya.

Aidha, ilielezwa kuwa serikali za majimbo zina ridhaa ya kujiamulia zenyewe kama zitahitaji uvaaji wa barakoa katika maeneo ya ndani yanayofikiwa na umma wa watu.

Pia baadhi ya maofisa wa majimbo walisema bado kuna mengi yanapaswa kujadiliwa ili kuhakikisha suala hilo linafikia hatua nzuri za maelewano kwa kufuata hatua zote muhimu za upendekezaji wa sheria hiyo.

**DW**



Rais Uhuru Kenyatta akipiga kura katika uchaguzi mkuu uliofanyika nchini humo jana. **PICHA: PSCU.**

# Kenyatta atoa neno baada ya kupiga kura

**NAIROBI,** KENYA

RAIS Uhuru Kenyatta ameelezea imani yake katika mchakato wa uchaguzi baada ya kupiga kura katika eneo la bunge la Gatundu Kusini, kaunti ya Kiambu.

Akizungumza na vyombo vya habari baada ya kupiga kura jana, Rais Kenyatta, alisema kuwa shughuli hiyo ilikwenda vizuri, huku akiwataka Wakenya kujitokeza kwa wingi na kupiga kura.

Pia aliongeza kuwa Wakenya wanapaswa kuipa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) muda na nafasi ya kujumlisha na kutangaza matokeo.

"Ni kila Mkenya anatumai kuwa uchaguzi huu utakuwa huru na wa haki, mchakato ulikuwa mwepesi, sikuwapo kwa muda mrefu na mifumo ilionekana kufanya kazi, kwa hivyo tunatumai itaendelea hivyo kwa siku nzima," alisema Kenyatta.

"Hii ni siku ya kupiga kura na tunaomba kwamba Wakenya wajitokeze kupiga kura kwa amani na kurejea nyumbani kusubiri matokeo," alisema Kenyatta.

Uhuru aliambatana na Mke wake Margaret Kenyatta, alisimama kwenye foleni pamoja na Wakenya wengine asubuhi ili kukamilisha suala la kupiga kura.

Awali Mama Nginna Kenyatta, alijiunga na maelfu ya wananchi wa Gatundu Kusini katika kutekeleza haki yake ya kidemokrasia, huku akitoa wito kwa wakenya kuwachagua viongozi sahihi.

"Wakati kila mpiga kura halali anashiriki katika mchakato wa kupiga kura, tunaweka mamlaka kwa watu wanaofaa kuongoza nchi hii.

"Ni muhimu kwa kila mtu kuelewa umuhimu wa kupiga kura," alisema Ngina.

**"Ni kila Mkenya anatumai kuwa uchaguzi huu utakuwa huru na wa haki, mchakato ulikuwa mwepesi, sikuwapo kwa muda mrefu na mifumo ilionekana kufanya kazi, kwa hivyo tunatumai itaendelea hivyo kwa siku nzima," alisema Kenyatta.**

Kiongozi wa taifa, mke wake na mama yake ni miongoni mwa viongozi wakuu na maofisa wa serikali ambao walipiga kura.

Viongozi wengine mashuhuri walioshiriki katika zoezi hilo ni pamoja na Naibu Rais William Ruto, mgombea mwenza wake Rigathi Gachagua, mgombea mwenza wa Azimio la Umoja Martha Karua, Waziri wa Mambo ya Ndani Fred Matiang'i na Katibu Mkuu wake, Karanja Kibicho.

Aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga na mkewe, Mama Ida, wameratibiwa kupiga kura katika eneo bunge la Kibra.

**WAGOMBEA WAKUU WAPIGA KURA**

Wagombea wakuu wa urais katika uchaguzi huo Raila Odinga, William Ruto, Waihige Mwaura walitekeleza wajibu wao wa kupiga kura, ambapo Naibu Rais Ruto wa Chama cha UDA alipiga kura nyumbani kwake eneo la Sugoi lililopo jimbo la Bonde la Ufa.

Raila Odinga na mgombea mwenza Martha Karua walipiga kura katika eneo la bunge la Gichugu lililopo Kirinyaga.

Mgombea mwenza wa Ruto, Rigathi Gachagua, alipiga kura katika eneo la bunge la Mathira.

Mgombea wa urais wa Chama cha Roots Prof. Wajakoya, kwa mujibu wa BBC alikutana na changamoto za kielektroniki za kifaa cha kupigia kura cha KIEMS katika kituo cha kupigia kura cha Shule ya Msingi ya Indangalasia ambapo baadae alipiga baada ya tatizo kutatuliwa.

**KTN**

# M-BET YAFURAHISHWA NA TAMASHA LA SIMBA DAY

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya M-BET Tanzania, imevutiwa na kufana kwa Tamasha la Klabu ya Simba (Simba Day), ambalo lilifanyika juzi Jumatatu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mbali ya utambulisho wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la Azam Federation na Ligi ya Mabingwa Afrika, tamasha hilo pia ni sehemu ya kusherehekea siku ya kuanzishwa kwa klabu hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko wa M-BET, Allen Mushi, ameliambia gazeti hili jana kuwa, wamefarijika jinsi tamasha hilo lilivyoandaliwa na kufanyika kwake kiasi cha mashabiki kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa unaoingiza jumla ya watu 60,000.

Mushi alisema M-BET ilikuwa inajumuika kwa mara ya kwanza tangu kuwa mdhamini mkuu wa klabu hiyo na jinsi mambo yalivyoendeshwa yalikuwa yenye ueledi wa hali ya juu.

"Ukiachana na changamoto mbalimbali, tamasha lilikuwa la kufana sana, mashabiki wengi walifiki na mbali ya kushuhudia timu hiyo ikishinda mabao 2-0, burudani za wasanii mbalimbali ziliwaburudisha mashabiki ambao walianza kuingia uwanjani kuanzia saa 2:00 asubuhi," alisema Mushi.

M-BET Tanzania imesaini mkataba wa miaka mitano na Klabu ya Simba wenye thamani ya Sh. bilioni 26.1 na kuwa wadhamini wakuu wa klabu hiyo.

Udhamini huo unaifanya Simba kuwa na thamani kubwa kuliko klabu zote nchini kutokana na kiasi kikubwa cha fedha. Mwaka wa kwanza wa mkataba wao, M-BET wataipa Simba Sh. bilioni 4.6 ambapo kiasi hicho kitaongezeka msimu wa pili na kuwa Sh. bilioni 4.9 na mwaka wa tatu wataipa Simba Sh. bilioni 5.2

M-BET itazidi kuiongezea Simba fedha kwani mwaka wanne wataipa Sh. bilioni 5.5 huku mwaka wa tano ikiipa kiasi cha Sh. bilioni 5.8.




Wachezaji wa Klabu ya Simba na St. George wakiingia uwanjani tayari kwa ajili ya kuanza mechi ya kirafiki iliyopigwa dimba la Benjamini Mkapa juzi na wenyeji kushinda mabao 2-0.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Warriors Queens tayari kwa michuano Caf

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Warriors Queens ya Zanzibar, inatarajiwa kuwasili Dar es Salaam leo tayari kwa ajili ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa Cecafa (Caf Women Champions League Cecafa Zone), inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Agosti 14, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Timu ya Warriors Queens ambayo ni mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar msimu huu, itaiwakilisha Zanzibar katika michuano hiyo ambayo inashirikisha nchi nane za Kanda ya Cecafa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Neema Machano Othman, alisema maandalizi yote yamekamilika kwa upande wa timu yao.

Alisema tayari wamekamilisha taratibu zote zinazohitajika kwa ajili ya ushiriki wao katika michuano hiyo ambayo inafanyika Tanzania Bara na kwamba licha ya ukata wa fedha walionao wana matumaini makubwa ya kufanya vizuri.

Alisema kwa upande wa kikosi chao, kocha amekiandaa vizuri kwa ajili ya kutoa ushindani, jambo ambalo linawapa matumaini ya kufanya vizuri.

"Kocha ameandaa kikosi kwa ajili ya kushindana na si kushiriki, ninamatumaini makubwa tutafanya vizuri na tutafikia lengo fulani ambalo tunahitaji, maana najua mashindano ni magumu na yanashirikisha mabingwa, hivyo na sisi tumejipanga vema," alisema.

Hata hivyo, alisema licha ya kwamba hii ni mara ya kwanza kwao kushiriki mashindano hayo ya kimataifa, lakini wachezaji wao wamehamasika ikiwamo ari ya kufanya vizuri kuwa juu.

# Mchengerwa mgeni rasmi 'NBC Patron Trophy'

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano maalum ya mchezo wa gofu yatakayojulikana kama 'NBC Patron Trophy', ambayo yatakuwa maalum kwa ajili ya kumuaga aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo.

Katika mashindano hayo yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 27, mwaka huu, Benki ya NBC imetoa kiasi cha Sh. milioni 10 kwa Klabu ya Gofu Lugalo ili kufanikisha maandalizi hayo huku yakitarajiwa kufanyika viwanja vya Lugalo, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema mashindano hayo ni maalum kwa ajili ya kumuaga mlezi wao, Mabeyo ambaye alikuwa na mchango mkubwa katika sekta ya michezo. Alisema Mchengerwa atakuwa mgeni rasmi katika mashindano hayo ambayo pia yatatumika kumkaribisha mlenzi wao mpya, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda.

"Tunatarajia Mchengerwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano hayo ya kumuaga Mabeyo ambaye alikuwa na mchango mkubwa katika sekta ya michezo kwa JKT na mchango mkubwa kwa Taifa katika michezo ikiwamo gofu, soka na ngumi," alisema Luwongo.

Alisema wamealika wachezaji kutoka klabu zote za hapa nchini ikiwamo Moshi Klabu, Arusha Gymkhana, Klabu ya Mufindi, Morogoro Gymkhana, Dar es Salaam Gymkhana, Sea Cliff Gofu Zanzibar, Kili Gofu na TPC Gofu.

"Mashindano hayo ya siku moja yatajumuisha wachezaji wa ridhaa kwa maana ya DIV A, B, C, Senior, wanawake na watoto," alisema Luwongo.

Alisema klabu hiyo imejiandaa vizuri kwa ajili ya kuendesha mashindano hayo ikiwa ni pamoja na maboresho makubwa ya viwanja.

Naye Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema katika mwendelezo wao wa kuchangia michezo ametoa Sh. milioni10 kwa ajili ya kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika.

## ZISIKUPITE

### RABIOT HUYOOO UNITED
KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano na Juventus juu ya ununuzi wa kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27 kwa dau la awali la pauni milioni 15. ***(Guardian)***

### ARSENAL YAMTAKA PINO
ARSENAL na Liverpool zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Hispania, Yeremi Pino mwenye umri wa miaka 19 kutoka Villarreal. ***(AS)***

### BROZOVIC ALENGWA LIVERPOOL
KIUNGO wa kati wa Inter Milan na Croatia, Marcelo Brozovic mwenye umri wa miaka 29, ndiye anayelengwa na Liverpool kama kiungo wa kati wa dharura. ***(Sport)***

### RODRIGUEZ AULIZIWA UNITED
MANCHESTER United pia wamemuulizia kiungo wa kati wa Real Betis na Argentina, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 28. ***(AS)***

### WERNER SAFI LEIPZIG
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26, jana Jumanne alifanyiwa vipimo vya afya yake kabla ya kurejea RB Leipzig. ***(Mail)***

### ROMA WAIKATALIA SPURS
AS Roma wamekataa ombi la Tottenham Hotspur la kumnunua winga wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo. ***(90min)***

### SAVIC ANYATIWA OLD TRAFFORD
KIUNGO wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27, pia bado yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaonyatiwa na Manchester United. ***(Telegraph)***

### DIOP MIAKA MITANO
KLABU ya West Ham imekubali ofa ya pauni milioni 15 kutoka kwa Fulham kwa ajili ya mlinzi wa Ufaransa, Issa Diop, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akitarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano. ***(Mail)***

### DENAYER KUTUA FULHAM
FULHAM wamepewa ofa ya beki wa Ubelgiji, Jason Denayer mwenye umri wa miaka 27, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Lyon kumalizika. ***(Football insider)***

### SESKO AWINDWA MAN U
MCHEZAJI mwingine anayelengwa na Manchester United ni mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 19, ambaye anakaribia kukubali mkataba wa kujiunga na RB Leipzig kutoka Red Bull Salzburg. ***(90min)***




# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FOFANA AKARIBIA KUTUA CHELSEA

**Leicester imeripotiwa kuwa tayari kumuuza kama watatoa ofa ya pauni milioni 80, hivyo...**

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea inajiamini kwamba, itaweza kufikia makubaliano ya kumsajili beki wa kati wa Leicester City, Wesley Fofana, kwa mujibu wa 90min.

'The Blues' hao tayari wamewanunua Kalidou Koulibaly na Marc Cucurella msimu huu wa majira ya joto, lakini wanataka kuongeza mlinzi mmoja wa kati, huku Fofana sasa akiwa katika nafasi ya juu kwenye orodha ya wanaowaniwa.

Leicester mara kadhaa imeripotiwa kutokuwa tayari kumuuza mlinzi huyo, lakini wako tayari kufanya biashara ikiwa Chelsea watatoa ofa ya pauni milioni 80.

Ofa ya hivi karibuni ya Chelsea ilikuwa na thamani ya pauni milioni 70, ambayo Leicester waliikataa, lakini vyanzo vya karibu vya ndani vimefichua kuwa kuna matumaini kutoka kwa The Blues kwamba makubaliano ya jumla hayako mbali kufikiwa.

Chelsea wamejaribu kujadili punguzo kwa kutoa wachezaji badala yake, lakini Leicester wameshikilia msimamo wa kutaka fedha ndefu.

Mazungumzo bado yanaendelea na Fofana, pamoja na beki huyo, Chelsea pia wanataka kuleta beki mwingine wa kulia ili kutoa ushindani kwa Reece James msimu huu. Beki mkongwe Cesar Azpilicueta amejitolea kusalia Chelsea, lakini hivi majuzi alizungumza kuhusu ugumu wake kucheza kama beki wa pembeni chini ya kocha Thomas Tuchel.

Denzel Dumfries wa Inter anasalia kuwa chaguo la Chelsea katika nafasi hiyo, lakini wasiwasi juu ya bei ya Mholanzi huyo umewafanya waulize kuhusu Kyle Walker-Peters wa Southampton.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/-
1,021,2

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 11 NA 12 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/08/22 | 17:00 | Tobol Kostanay vs Zrinjski Mostar | 2.52 | 3.27 | 2.72 |
| 02. 11/08/22 | 19:00 | Chojnice vs ZKS Stal Rzeszow | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 11/08/22 | 19:30 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.29 | 2.82 | 3.52 |
| 04. 11/08/22 | 20:30 | Panathinaikos vs Slavia Prague | 2.44 | 3.13 | 2.93 |
| 05. 11/08/22 | 21:00 | KI Klaksvik vs KF Ballkani | 2.23 | 3.38 | 3.08 |
| 06. 11/08/22 | 21:00 | Shkendija vs AIK Football | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 07. 11/08/22 | 21:00 | Hibernians vs Rigas Futbola Skola | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 08. 11/08/22 | 22:00 | West Bromwich vs Sheffield Utd | 2.24 | 3.26 | 3.11 |
| 09. 12/08/22 | 01:00 | Mvo Wanderers vs CA Fenix | 2.28 | 3.17 | 3.17 |
| 10. 12/08/22 | 05:00 | Queretaro FC vs San Luis | 2.26 | 3.21 | 3.11 |
| 11. 12/08/22 | 18:30 | IF Gnistan vs FF Jaro | 2.92 | 3.51 | 2.26 |
| 12. 12/08/22 | 19:00 | Miedz Legnica vs Zaglebie Lubin | 2.46 | 3.15 | 2.66 |
| 13. 12/08/22 | 19:30 | Kaiserslautern vs Paderborn | 2.54 | 3.43 | 2.54 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ISCO RASMI MALI YA SEVILLA



**SEVILLE, Hispania**

KLABU ya Sevilla imekamilisha usajili wa Isco kwa uhamisho huru baada ya kiungo huyo wa kati wa Hispania kuondoka Real Madrid mwishoni mwa msimu uliopita.

Isco alitumia miaka tisa akiwa na Madrid, akishinda mataji matatu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika wakati wake pale Santiago Bernabeu.

Hata hivyo, baada ya kukosa namba, Isco aliondoka baada ya kumalizika kwa mkataba wake, na Sevilla Jumapili walifichua kuwa walikuwa wamefikia makubaliano kimsingi ya kumsajili kiungo huyo.

Klabu hiyo ya LaLiga Jumatatu ilithibitisha kuwa Isco amefuzu vipimo vyake vya afya, na leo Jumatano atatambulishwa kwenye Uwanja wa Ramon Sanchez-Pizjuan.

Anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na klabu hiyo kwenye dirisha la usajili baada ya Marcao kujiunga kutoka Galatasaray na Alex Telles kuwasili kwa mkopo kutoka Manchester United.

Isco alicheza chini ya Julen Lopetegui kwa muda mfupi akiwa Madrid, lakini alifanikiwa sana chini yake akiwa na timu ya taifa, akihusika katika mabao 11 katika mechi 14 alizoichezea Hispania kwenye mashindano yote.

# United yamnyakua Rabiot

**TURIN, Italia**

MANCHESTER United na Juventus zimefikia mabakubaliano ya ada ya pauni milioni 15 kwa ajili ya uhamisho wa Adrien Rabiot.

Ripoti zimeeleza kuwa Rabiot ambaye amekuwa na uhusiano mbaya na viongozi wa Juventus huku akibakisha mwaka mmoja katika mkataba wake, atajiunga na United iwapo pande hizo mbili zitafikia makubaliano ya vipengele binafsi.

Juventus ilimsajili Rabiot mwaka 2019 kwa uhamisho huru kutoka Paris Saint-Germain huku kiungo huyo akiamua kwa kushrikiana na mama yake anayetambulika kwa jina la Veronique, kwamba matarajio yake yalikuwa katika mikono bora mbali na mji mkuu wa Ufaransa.

Veronique anamwakilisha Rabiot na anasemekana kuwa katika mgongano na wachezaji wenzake na nyota huyo pamoja na wakurugenzi wa michezo, hivyo kutaka kukutana na makocha na kuhudhuria mazoezi kuhakikisha mwanawe anatendewa haki.

Manchester United inakabiliwa na tatizo la safu ya kiungo na uhamisho huo ni sehemu ya kutatua tatizo hilo.

Klabu hiyo imepoteza mchezo wake wa ufunguzi wa Ligi Kuu England 2022/23 na wa kwanza kwa kocha Erik ten Hag nyumbani dhidi ya Brighton & Hove Albion.



208,577/-

# OKWA ATAKA UBINGWA, ATUMA SALAMU YANGA

**Na Hadija Mngwai**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Simba, Mnigeria Nelson Okwa, ametuma salamu kwa wapinzani wao wa jadi, Yanga kwa kusema kuwa amekuja katika klabu hiyo ya Msimbazi kufanya kazi na kuahidi kuipigania ili kuipa ubingwa wa msimu ujao wa Ligi Kuu.

Okwa ambaye alionyesha uwezo mzuri katika mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Saint George SC ya Ethiopia juzi wakati Simba ikishinda kwa mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ndiye aliyefunga bao la pili akipokea pasi murua kutoka kwa Clatous Chama.

Simba iliutumia mchezo huo maalum katika Tamasha lao la Simba Day, kutambulisha wachezaji wake wa msimu ujao unaotarajiwa kuanza Agosti 17, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Okwa alisema amefurahishwa na mwitikio wa mashabiki uwanjani hapo na kudai kuwa amekuja kwa kazi moja tu ya kuhakikisha anaisaidia timu yake hiyo kutwaa ubingwa.

"Mechi ilikuwa nzuri St. George ni timu nzuri, ushindani ulikuwa mkubwa, bado sijakaa sawa kujuana na wachezaji wenzangu, natumai nitaendelea kujuana nao vizuri kadri tutakavyokuwa pamoja," alisema.

Aidha, kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, alisema," Okwa ni mchezaji mzuri na anacheza nafasi tatu au nne kwenye timu, anatoa pasi nzuri, anahitaji kuwekwa fiti zaidi kwa ajili ya kujiandaa na mechi zijazo".

Katika mchezo huo bao la kwanza lilifungwa na Kibu Denis kwa shuti kali baada ya kazi nzuri iliyoanzia kwa beki, Mohamed Quattara, kisha Agustino Okrah aliyemmegea Mohamed Hussein 'Tshabalala', kisha Habibu Kyombo akaugusa mpira kabla ya kumfikia mfungaji na kumaliza biashara mapema tu dakika ya 19.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mbeya City, Emmanuely Kimbe (wa pili kushoto), akishikilia jezi kwa pamoja na Ofisa Masoko wa Parimatch Africa, Ruby Chuku, katika hafla ya kampuni hiyo kutangaza rasmi kuidhamini timu hiyo ya Ligi Kuu nchini. Wengine katika picha ni Ofisa Habari wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed (kushoto) na Ofisa Uhusiano wa Mbeya City, John Kilua. **MPIGAPICHA WETU**

# Parimatch yaidhamini Mbeya City FC

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI inayoendesha shughuli za Michezo ya Kubashiri Mtandaoni ya Parimatch Tanzania, imeingia makubaliano ya mkataba wa udhamini na Klabu ya Mbeya City katika msimu ujao wa Ligi Kuu nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa kampuni hiyo, Imael Mohamed, alisema mkataba huo utahusisha kugharamia vifaa vyote vya michezo, usafirishaji na matengenezo madogo kwenye Uwanja wa Sokoine unaotumiwa na timu hiyo kwenye mechi zake nyumbani.

Kwa mujibu wa Mohamed, kampuni hiyo ilikuwa pia mdhamini wa klabu hiyo katika msimu wa 2020/2021 na wamerejea tena katika kujaribu kuiongezea zaidi nguvu msimu huu baada ya kuyumba msimu uliopita na kunusurika kushuka daraja.

"Mkataba huu unalenga kuwa wa manufaa kwa pande zote mbili, ikitiliwa maanani kwamba Mbeya City ni moja ya timu zenye mashabiki wengi nchini. Kwa hiyo ni faraja kwetu kuingia nayo mkataba ili kuzidi kuiongezea nguvu msimu ujao," alisema Mohamed.

"Mbali na kuiongezea nguvu Mbeya City, mkataba huu pia ni jitihada za kuendeleza mchezo wa soka nchini na kuunga mkono juhudi za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF)."

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mbeya City, Emmanuely Kimbe, aliishukuru Kampuni ya Parimatch kwa niaba ya wakazi wa Halmashauri ya Mbeya kwa kufikiwa kwa makubaliano na kusema yatakuwa ni msaada mkubwa kwao.

"Ligi Kuu ina gharama sana kwa timu na msimu uliopita tulicheza bila mdhamini, hivyo kuna wakati tuliyumba kidogo, lakini udhamini huu utakuwa ni msaada mkubwa sana kwetu katika harakati za kuirudisha Mbeya City katika kiwango chake," alisema Kimbe.

Akizungumza pia wakati wa hafla hiyo, Ofisa Masoko wa Parimatch Africa, Ruby Chuku, alisema kampuni yao imefurahishwa na makubaliano hayo na watatimiza yote waliyokubaliana bila matatizo yoyote.

"Tunajua Afrika soka ndiyo mchezo maarufu zaidi, lakini tunaweza kuangalia pia uwezekano wa kudhamini michezo mingine kama tenisi na ngumi pale panapokuwa na fursa ya kufanya hivyo," alisema Chuku.

## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/2022 | 17:00 | Brighton vs Newcastle | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 02. 13/08/2022 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.24 | 3.39 | 3.09 |
| 03. 13/08/2022 | 17:00 | Wolverhampton vs Fulham | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 04. 13/08/2022 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 13/08/2022 | 17:00 | Sunderland vs QPR | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 06. 13/08/2022 | 17:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.28 | 2.98 |
| 07. 13/08/2022 | 21:45 | AC Monza Brianz vs Torino | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 08. 14/08/2022 | 13:15 | FC Volendam vs NEC Nijmegen | 2.53 | 3.47 | 2.63 |
| 09. 14/08/2022 | 15:00 | Viborg FF vs Silkeborg IF | 2.83 | 3.48 | 2.36 |
| 10. 14/08/2022 | 16:00 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 11. 14/08/2022 | 16:00 | Troyes vs Toulouse | 2.58 | 3.17 | 2.73 |
| 12. 14/08/2022 | 16:00 | AJ Auxerre vs Angers | 2.28 | 3.11 | 3.21 |
| 13. 14/08/2022 | 16:30 | Mainz vs Union Berlin | 2.29 | 3.26 | 3.06 |
| 14. 14/08/2022 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 15. 14/08/2022 | 18:05 | Nice vs Strasbourg | 2.23 | 3.21 | 3.21 |
| 16. 14/08/2022 | 18:30 | Chelsea vs Tottenham | 2.22 | 3.33 | 3.18 |
| 17. 14/08/2022 | 18:30 | Cadiz CF vs Real Sociedad | 3.13 | 3.13 | 2.35 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 10 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3241 | Yokohama F Marinos vs Sanfrecce Hiroshima | 2.03 | 3.64 | 3.00 |
| 13:00 | 3278 | Kawasaki Frontale vs Cerezo Osaka | 1.97 | 3.35 | 3.40 |
| 13:00 | 3508 | Suwon City vs Jeonbuk Hyundai | 3.00 | 3.29 | 2.16 |
| 13:00 | 4661 | Avispa Fukuoka vs Vissel Kobe | 2.79 | 2.94 | 2.50 |
| 13:30 | 2007 | Gangwon vs Daegu | 2.26 | 3.25 | 2.85 |
| 13:30 | 3998 | Urawa Red Diamonds vs Nagoya Grampus | 1.99 | 3.08 | 3.67 |
| 14:45 | 5061 | Albirex Niigata (SIN) vs Young Lions | 1.07 | 9.05 | 17.70 |
| 16:00 | 2304 | Uitm FC vs Projek Fam-Msn | 1.52 | 3.87 | 5.48 |
| 16:00 | 3050 | Terengganu vs Johor Darul Takzim | 6.30 | 4.43 | 1.40 |
| 17:00 | 4685 | Otmk Olmaliq vs Lokomotiv Tashkent | 2.03 | 3.00 | 3.64 |
| 17:30 | 5990 | Al Gharafa SC vs AL Wakrah | 3.63 | 3.78 | 1.79 |
| 18:00 | 3721 | FK Minija vs FK Vilnus Bfa | 2.86 | 3.55 | 2.13 |
| 18:00 | 3914 | Amazulu vs SuperSport Utd | 2.20 | 2.85 | 3.60 |
| 18:00 | 4726 | Bunyodkor vs Qizilqum | 2.06 | 3.05 | 3.49 |
| 18:00 | 5763 | Zaglebie II Lubin vs Lech II Pozna | 2.34 | 3.33 | 2.69 |
| 18:30 | 2567 | FC Vaajakoski vs JJK Jyvaskyla | 6.89 | 4.82 | 1.34 |
| 19:00 | 1296 | Vitoria Guimaraes vs Hajduk Split | 2.39 | 3.23 | 2.93 |
| 19:00 | 3968 | Zaglebie Sosnowiec vs GKS Tychy | 2.33 | 3.33 | 2.69 |
| 19:00 | 4645 | Resovia Rzeszow vs Arka Gdynia | 2.84 | 3.19 | 2.30 |
| 19:30 | 2476 | Smouha Club vs Coca Cola | 3.21 | 3.26 | 2.19 |
| 19:30 | 5787 | Arab Contractors vs El Gouna | 2.14 | 2.96 | 3.71 |
| 19:40 | 3959 | Al-Sailiya SC vs Al-Shamal | 1.85 | 3.63 | 3.53 |
| 20:00 | 1058 | Wehen vs Bayreuth | 1.69 | 3.75 | 4.50 |
| 20:00 | 2754 | Dynamo Dresden vs Verl | 1.64 | 3.79 | 4.89 |
| 20:00 | 3574 | Germany W U20 vs Colombia W U20 | 1.11 | 7.45 | 15.69 |
| 20:00 | 3709 | UMF Selfoss vs Thor Akureyri | 2.06 | 3.73 | 2.89 |
| 20:00 | 4490 | Osnabruck vs Ingolstadt | 2.40 | 3.26 | 2.81 |
| 20:00 | 4974 | FC Luzern vs Grasshoppers | 1.78 | 3.77 | 4.02 |
| 20:00 | 5359 | Saarbrucken vs Borussia Dortmund II | 1.91 | 3.50 | 3.70 |
| 20:30 | 2688 | Stellenbosch vs Orlando Pirates | 3.50 | 2.80 | 2.29 |
| 20:30 | 3195 | Chippa Utd vs Bloemfontein Celtic | 3.10 | 2.90 | 2.42 |
| 20:30 | 3789 | Sekhukhune United vs Golden Arrows | 2.75 | 2.75 | 2.84 |
| 20:30 | 4000 | Mamelodi Sundowns vs TS Galaxy FC | 1.44 | 4.10 | 7.01 |
| 20:30 | 4640 | Memmingen vs TSV 1860 II | 1.79 | 3.55 | 4.20 |
| 21:30 | 3456 | LKS Lodz Pss vs Puszcza Niepolomice | 1.98 | 3.29 | 3.44 |
| 21:45 | 1891 | Blackburn vs Hartlepool | 1.36 | 4.82 | 7.43 |
| 21:45 | 3073 | Plymouth vs Peterborough | 2.25 | 3.47 | 2.92 |
| 21:45 | 3214 | Middlesbrough vs Barnsley | 1.40 | 4.62 | 7.03 |
| 21:45 | 3930 | Port Vale vs Rotherham | 3.27 | 3.22 | 2.18 |
| 21:45 | 4015 | Coventry vs Bristol City | 1.95 | 3.46 | 3.66 |
| 21:45 | 5938 | Sheffield Wed vs Sunderland | 2.56 | 3.26 | 2.66 |
| 22:00 | 5667 | Real Madrid vs Eintracht Frankfurt | 1.42 | 4.41 | 5.88 |
| 22:15 | 4942 | HK Kopavogs vs Throttur Vogum | 1.22 | 6.11 | 8.47 |
| 01:00 | 2995 | Nautico PE vs CRB AL | 2.29 | 2.99 | 3.04 |
| 01:00 | 5368 | Chapecoense vs Novorizontino SP | 2.46 | 2.86 | 2.91 |
| 01:15 | 5190 | Ceara CE vs Sao Paulo | 2.37 | 2.95 | 2.95 |
| 02:00 | 4227 | Spain W U20 vs Brazil W U20 | 1.65 | 3.72 | 4.41 |
| 03:30 | 4541 | Criciuma SC vs Guarani SP | 2.02 | 2.96 | 3.75 |
| 03:30 | 5066 | Talleres vs Velez Sarsfield | 2.21 | 2.99 | 3.19 |
| 03:30 | 5878 | Palmeiras vs Atletico Mineiro | 1.75 | 3.25 | 4.53 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatano Agosti 10, 2022

Nipashe



## Fofana akaribia kutua Chelsea

AMERUDI AISEE...





Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akiichekecha safu ya ulinzi ya Saint George ya Ethiopia kabla ya kutoa pasi ya mwisho kwa Nelson Okwa aliyeifungia timu yao bao la pili kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na wenyeji hao kushinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA PAGUMU CAF, YANGA KWA VIBONDE

## ●●●Zikivuka tabu iko palepale, kuzivaa De Agosto na Al Hilal ya Ibenge, makocha wafunguka....

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wamepangwa kucheza dhidi ya Zalan ya Sudan Kusini, huku Simba iliyoishia Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ikipewa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwenye mechi za awali Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Wakati vigogo hao wakipangiwa timu hizo, Geita Gold ambayo msimu huu itacheza kwa mara ya kwanza michuano ya kimataifa, imepangwa kucheza dhidi ya Hilal Alsahil ya Sudan, huku Azam FC ambayo haitocheza mechi za awali, itasubiri mshindi kati ya Al Akhdar ya Libya dhidi ya Al Ahli Khartoum ya Sudan.

Kwa mujibu wa droo iliyopangwa jana jijini Cairo, Misri, iwapo Yanga itafanikiwa kuitoa Zalan, itakipiga na mshindi kati vibonde wa Simba kwenye mechi ya kirafiki, Saint George ya Ethiopia dhidi ya Al Hilal ya Sudan inayonolewa na kocha wa zamani wa Berkane ya Morocco, Florent Ibenge.

Kwa upande wa Simba kama itawatoa Wamalawi hao, itakumbana na mshindi kati ya Premiero de Agosto ya Angola dhidi ya Red Arrows ya Zambia.

Timu ya Geita Gold kama itafanikiwa kuvuka mtihani huo, itakuwa na kazi nyingine nzito ya kuivaa Pyramids ya Misri.

Kati ya timu hizo, Zalan, Hilal Alsahil, Al Akhdar na Al Ahli Kartoum zote ni ngeni kwenye macho na masikio ya mashabiki wa soka Tanzania, lakini zilizobaki zimeshawahi kutua nchini kucheza mechi mbalimbali za kimataifa na mashindano ya kirafiki. Timu inayokutana na Simba ilitua nchini kucheza michuano ya Kombe la Kagame 2021, ikafungwa kwenye hatua ya fainali bao 1-0 dhidi ya Express ya Uganda kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Timu ya Al Hilal iliwahi kufika nchini kwenye michuano maalum ya Simba msimu uliopita, na Jumatatu iliyopita St. George ilikuwa nchini ikicheza dhidi ya Simba kwenye kilele cha Simba Day, ikachapwa mabao 2-0.

Red Arrows ilicheza dhidi ya Simba kwenye Kombe la Shirikisho mwaka jana, ikafungwa mabao 3-0 Wekundu wa Msimbazi wakishinda nyumbani Novemba 28, na Desemba 5, ikichapwa mabao 2-1, lakini bao la ugenini likawavusha.

Pyramids iliwahi kucheza dhidi ya Azam na Namungo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, na Primero de Agosto pia iliwahi kucheza dhidi ya Namungo. Mechi za kwanza zitapigwa kati ya Septemba 9-11 na kurudiana kati ya Septemba 16-18, mwaka huu huku Simba na Yanga zote zikianzia ugenini.

Akizungumza na Nipashe baada ya droo hiyo kupangwa jijini Cairo Misri jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola alisema hawataidharau timu yoyote kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Big Bullets ni timu nzuri pia wanauzoefu mkubwa wa michuano ya kimataifa, hatuwadharau kwa sababu msimu uliopita tumepata funzo kwa kutokea mapema na timu kutoka nchini Botswana (Jwaneng Galaxy).

"Kwa sababu hiyo hatutaichukulia poa sana Big Bullets kwa sababu malengo yetu bado yako pale pale ya kuhakikisha tunaenda kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lazima kushinda mechi katika kila hatua," alisema Matola.

Kwa upande wa Yanga, kupitia Mkurugezi wa Mashindano wa klabu hiyo, Saad Kawemba, alisema akili na nguvu zao ziko katika mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya Simba.

Alisema ratiba hiyo na kuhusu Zalan FC ya Sudan watakaocheza nao, hawaifikiria kwa sababu muda uliopo kwa sasa wanafikiria Ngao ya Jamii dhidi ya Simba Jumamosi.

"Hiyo ratiba kwa sasa hatuwezi kuizungumzia wala huyo mpinzani wetu kwa sasa, kwa sababu kabla ya mchezo huo tuna mechi ya Jumamosi dhidi ya Simba," alisema Kawemba.

## Zoran awatoa hofu Simba kwa Yanga

**Na Saada Akida**

LICHA ya kukiongoza kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Saint George ya Ethiopia juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, amewasifu wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri, lakini akasema bado anahitaji kukisuka zaidi kwa ajili ya kuwa bora zaidi.

Simba ambayo iliibuka na ushindi huo katika mechi hiyo ya kirafiki maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wake wa msimu mpya iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, itaanza rasmi kampeni yake ya kusaka mataji dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga kwenye mechi ya Ngao ya Jamii ya kukaribisha msimu wa 2022/23 itakayopigwa Jumamosi uwanjani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zoran Maki, alisema mechi hiyo imemsaidia kuona mapungufu na ubora wa kikosi chake, lakini bado anahitaji kukisuka zaidi ili kuwa imara kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema licha ya kucheza na kupata ushindi ameona mapungufu ya kikosi chake na atayafanyia kazi kuhakikisha wanakuwa imara zaidi kabla ya mchezo wao wa Ngao ya Jamii, Jumamosi dhidi ya Yanga.

"Nimefurahi kwa matokeo mazuri wachezaji wameonyesha kile nilichowapa katika uwanja wa mazoezi, mapungufu nimeyaona katika ufundi na mbinu nitahakikisha tunakuwa vizuri na tayari kwa ajili ya mchezo wetu wa 'Derby' dhidi ya Yanga," alisema Zoran.

Alisema hawezi kuhofia mchezo huo wa Derby kwa sababu ya uimara wa kikosi chake na kwamba atahakikisha wanaendelea kuwapa furaha mashabiki wa Simba, kushinda mechi ijayo na kutwaa taji la Ngao ya Jamii.

Zoran Maki alisema malengo na mikakati yao mikubwa ni kuhakikisha wanaanza vizuri Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwamo kushinda mchezo wao huo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Saint George, Zerihun Shengeta, amewataja Pape Sakho na Augustine Okrah kwamba walikuwa mwiba mchungu sana kwake katika mchezo huo wa kirafiki.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >